

Samia akamilisha

4

Miaka ya Rais Samia aliyokaa madarakani, amefanya mageuzi makubwa katika sekta ya afya, miundombinu, elimu bure, kuongeza kiwango cha fedha za mikopo ya wanafunzi, kilimo na kukamilisha miradi mikubwa ya kimkakati

Rais Samia Suluhu Hassan



Habari Uk. 6&7

Bangi ya Malawi yaliza Watanzania

● **Mmoja apoteza milioni 700/-**

TAMAA ya kuingiza fedha nyingi kupitia kilimo cha bangi baada ya kuhalalishwa nchi jirani ya Malawi, imewaponda baadhi ya wafanyabiashara... **Habari Uk. 4**

TAHARIRI

Tusizoeshwe risasi

Uk. 2



Tahariri/Katuni

Tusizoeshwe risasi, mabomu, virungu

JANA Jumapili – Juni 29, 2025 - damu ya baadhi ya watu wanaonekana kuwa kwenye mkusanyiko wa maombi, ilimwagika, baada ya kutokea rabsha kati yao na askari wa Jeshi la Polisi.

Siyo siri, wala haikuwa kizani, kwamba Watan-zania waliona kilichokuwa kikitokea katika eneo la Ubungo Maziwa, Dar es Salaam, ambako waumini wa Kanisa la Ufufuo na Uzima walikusanyika kwa ajili ya maombi, lakini ibada yao ikageuka kuwa shubiri baada ya kuvamiwa na askari wa Jeshi la Polisi.

Askari hao inaelezwa kuwa walifika kwa ajili ya kumkamata mmoja wa viongozi wa kiroho wa kani-sa hilo, Askofu Maximillian Machumu, almaarufu Mwanamapinduzi, ambaye alikuwa kwenye jumui-ko hilo.

Hata hivyo, waumini nao hawakukubali na bada-la yake wakashauri kwamba kiongozi huyo aach-we afanye ibada na baada ya ibada ataenda kokote atakapotakiwa kwenye vyombo vya usalama.

Inaelezwa kuwa baada ya majibizano ya muda, askari hao walianza kumburuta Askofu Mwana-mapinduzi, hatua ambayo waumini hawakuona kuwa ni busara. Wakazidi kung'ang'ana asibututwe, bali apewe haki yake ya kuabudu kwanza.

Katika rabsha hiyo, polisi walitumia mabomu ya machozi kutawanya hadhira iliyokuwa ikipinga

walichokuwa wakifanya polisi na miongo-ni mwao, waumini kadhaa walijeruhiwa, mmoja wao akiwa na hali mbaya baada ya kuvuja damu nyingi kichwani.

Sisi Pambazuko tunapinga na kulaani kwa nguvu zote kuvamiwa na hata kupig-wa kwa waumini waliokuwa wakiendelea na ibada ya kuomba kwa Mungu.

Kwa muda sasa, waumini wa kanisa hilo, maarufu – Kanisa la Gwajima - kuto-kana na jina la kiongozi wao mkuu, Askofu Josephat Gwajima, wamekuwa wakiende-sha ibada zao nje ya kanisa lao, baada ya kuwepo kwa uamuzi wa kulifunga kanisa hilo kutoka kwenye mamlaka - serikalini.

Pambazuko tunaamini kuwa pamoja na kuwepo kwa katazo hilo la kufika kanisani, lakini hakuna namna waumini hao wa-naweza kuzuiwa kutenda kwa imani yao; kufanya ibada; hata iwe ndani ya kanisa jingine, ilimuradi wanaohusika wame-kubaliana kumuomba Mungu wao kwa pamoja.

Yaliyoshuhudiwa jana wakati wa kud-hibiti waumini hao wa Kanisa la Gwajima, ni kujiongoza vibaya kwa “wakubwa wetu” na hata kuwepo kwa matumizi makubwa na mabaya ya silaha – kurusha mabomu ya machozi, rasilimali watu –ya askari na kupoteza muda ambao ungeweza kutu-mika kwa shughuli zingine za kudhibiti madhila mengine, na kamwe siyo ibada.

Kuendelea kuwepo kwa mazoea ya kutumia silaha na vipigo, kwa wananchi, siyo hatua njema yenye afya, isipokuwa ni mwanzo wa kujenga mazoea mabaya kwa Watanzania juu ya vifaa na rasilimali za kuwalinda.

Ni vyema sasa vyombo vyetu vya usala-ma, vikaendelea kujenga taswira kwam-ba vipo kwa ajili ya kulinda wananchi na mali zao, badala ya kuonekana vyombo vya mabavu, kuonea na hata kuminya haki zinazopaswa kuheshimiwa na kila mmoja.



Ajali zimezidi...



Wananchi wakiangalia ajali iliyohusisha magari matatu ikiwemo gari la wanafunzi baada ya daladala kupoteza mwelekeo na kugonga magari hayo na kusababisha vifo vya watu wawili eneo la Kimara Suka jijini Dar es Salaam juzi. Picha na Fidelis FELIX

Jisajili kupata Pambazuko bure

- Ndugu msomaji wetu, jisajili kwa namba hii ya simu ya **WhatsApp: +255 744 768263** kwa kutuma neno **“HABARI”** kwa namba yako ya WhatsApp ili kupata Pambazuko kwenye WhatsApp yako.

- Pia unaweza kujisajili kwa kutumia **Email hii: info@pambazuko.or.tz** ili gazeti la Pambazuko likufikie kupitia email yako, andika neno **“HABARI”** na kutuma kwetu nawe utakuwa umejisajili.

Unaweza kusoma gazeti hili kupitia tovuti ya **www.rifaly.com**

TIMU YA PAMBAZUKO

Mhariri Mkuu	:	Simon MKINA	(simon@pambazuko.or.tz)
Mhariri Mtendaji	:	Peter NYANJE	0784 211 716
Mhariri wa Habari	:	Arodia PETER	0783 682 018
Mwandishi Mkuu	:	Elizabeth HOMBO	0712 792 216
Mwandishi Mwandamizi	:	Andrew MSECHU	0769 415 815
Mkuu wa DTP	:	Yassin LUPATU	0782 009 971
Mkuu wa Utawala	:	Tryruckia MFINANGA	0744 768 263

Tunapatikana Pambazuko Initiative Office, Mtaa wa Mpakani A - nyuma ya Jengo la Sayansi. Kitalu Namba 435; Plot 44. Mawasiliano ya ofisi: Simu +255 744 768263 na Email: info@pambazuko.or.tz

Habari

Bangi ya Malawi yaliza Watanzania

**Na Waandishi WETU**

TAMAA ya kuingiza fedha nyingi kupitia kilimo cha bangi baada ya kuhalalishwa nchi jirani ya Malawi, imewaponda baadhi ya wafanyabiashara wa Tanzania, Uchunguzi wa Pambazuko umebaini.

Uchunguzi wa gazeti hili uliofanywa kwa zaidi ya mwezi mmoja sasa, umebaini kuwepo kwa Watanzania wanane ambao walijitosa kwenye biashara hiyo tangu mwaka 2022, miaka miwili baada ya Malawi kuruhusu kilimo cha bangi.

Pambazuko limegundua kuwepo kwa wafanyabiashara wa Tanzania watatu waliowekeza mitaji yao katika eneo la Milima ya Likwakwa, wilayani Mzimba, ambako ndiko kuna kilimo kikubwa cha zao hilo lililoharamishwa Tanzania.

Watanzania wengine wanne wakiwekeza mitaji yao katika eneo lililoko pembezoni mwa Mto Lupache, wilayani Nkotakota ambako bangi hulinwa kwa wingi pia.

Mmoja wa raia wa Tanzania alikuwa eneo la Kasungu, nje kidogo ya Mji Mkuu wa Malawi, Lolingwe. Huyu aliwekeza kiasi kidogo ikilinganishwa na wengine.

Pamoja na kwamba “wawekezaji” hawa hawamo kwenye vitabu vya usajili, lakini Pambazuko limeelezwa na wawili ambao limekutana na kuzungumza nao kwa masharti ya kutotajwa majina yao gazetini.

Wawili hao walitaja majina ya wenzao, na

mahali walikokuwa wakifanya shughuli zao, lakini Pambazuko haliwezi kuwataja kwa kuwa halikufanikiwa kuwapata kuzungumza nao.

Mmoja wao inaelezwa kuwa alipoteza kiasi cha Shilingi milioni 700, baada ya kuziwekeza kwenye kilimo hicho, lakini mwaka jana, biashara “ikagoma.”

Mfanyabiashara huyo ameelezwa kuwa ni Mkazi wa Dar es Salaam, ambaye amekuwa akifanya shughuli za kuuza matairi ya magari makubwa, lakini aliamua kuingiza mtaji kwenye kilimo cha bangi Malawi tangu mwaka juzi – 2023 mwishoni.

Malawi yaruhusu bangi

Serikali ya Malawi iliruhusu kuanza kwa kilimo cha bangi, ikiwa ni jitihada zake kuinua uchumi, baada ya zao la tumbaku, kudorora.

Iliamuriwa na bunge la nchi hiyo Februari, mwaka 2020 kwamba kilimo hicho kianze, huku walengwa wakubwa wa kuendesha kilimo hicho wakitarajiwa kuwa wawekezaji wakubwa kutoka Ulaya na Amerika.

Pambazuko limeelezwa kuwa hadi kufikia Oktoba, 2021, kulikuwa na kampuni 72 ambazo zilikuwa zikijihusisha na kilimo na nyingine kujiandaa kwa ununuzi pekee.

Hata hivyo, hadi Juni 18, ni kampuni 37 tu zilizokuwa na leseni zilizohuishwa, huku zingine zikikwama kuendelea na biashara hiyo. Hakuna kampuni iliyobainika kumilikiwa na Mtanzania kihalali.

Biashara na kilimo cha bangi kiliruhusiwa Malawi, siyo kwa kuvuta ndani ya nchi hiyo, bali matumizi ya kitabibu; ikiwamo tiba na kichocheo cha nusu kaputi, na kutumika kwa mambo mengine nje ya nchi hiyo.

Watanzania waingiaje?

Miaka miwili baada ya biashara ya kilimo cha bangi kushamiri nchini Malawi, huku wakulima wakipata mamilioni ya fedha, baadhi ya Watanzania wanaofanya biashara nchini humo, waliamua kuvamia kilimo cha bangi, huku wengine wakialika ndugu zao kujiunga nao ili “kupiga pesa.”

Dunia: Hapa na Pale

Acha kumshangaa Bezos!

TAJIRI namba tatu duniani, raia wa Marekani, Jeff Bezos (64) ametumia Shilingi bilioni 136 – kwa siku tatu; kuanzia Ijumaa hadi jana – Jumatapi, kwa ajili ya harusi yake ya pili.

Bezos, ambaye ni mmiliki wa kampuni kubwa ya Amazon na biashara zingine, Ijumaa iliyopita alifunga ndoa na mwandishi wa Lauren Sanchez (55). Harusi yao ilifanyika kwenye moja ya maeneo yenye gharama kubwa za misha duniani Venice, Italia.

Tajiri huyo alitalikiana na mkewe wa kwanza, MacKenzie Scott mwaka 2019 na kupata watoto wanne, huku Lauren akiwa na watoto watatu kutoka kwenye ndoa yake ya kwanza.



Mbunge aondolewa ulinzi

BABU Owino, ambaye ni Mbunge wa Embakasi Mashariki, Kenya, amelalamika kuondolewa kwa walinzi wake rasmi, akidai kuwa hatua hiyo imefuatia ushiriki wake kwenye maandamano yaliyofanyika nchini humo kupinga matukio ya utekaji na kuminywa kwa demokrasia.

Katika taarifa yake aliyoitoa Ijumaa iliyopita, mbunge huyo alisema hatua hiyo ya serikali ni uonevu na kwamba inalenga kudhoofisha juhudi zake kupigania haki na maendeleo ya Wakenya.

Babu anaeleza kuwa aliamua kuungana na idadi kubwa ya Wakenya kuandamana ili kuonyesha kuwa anakerwa kuona ama kusikia Wakenya wakitekwa ama kuuawa kwa kuwa tu wanakemea maovu yanayofanywa na serikali yao. Alisema kuwa kamwe hataacha kupigania haki.

Maiti 6,000 za wanajeshi

MIILI ya wanajeshi zaidi ya 6,000 waliouawa na majeshi ya Urusi, imekabidhiwa kwa Ukraine mwishoni mwa wiki, ikiwa ni sehemu ya kutekeleza makubaliano ya kumaliza vita na kukabidhiana wafungwa – wakiwamo wafu.

Waziri wa Ulinzi wa Ukraine, Rustem Umerov, amesema kuwa serikali yake imepokea jumla ya miili 6,057 hadi sasa kutoka Urusi, baada ya makubaliano hayo.

Urusi imesema iko tayari kukabidhi miili mingine 2,239 ya wanajeshi wa Ukraine, nje ya makubaliano ya awali, baada ya kuweka wazi kuwa hawa nao waliuawa kwenye vita kati ya mataifa hayo mawili iliyodumu kwa miaka takriban mitatu sasa.

Wapania kumuua Ayatollah

ISRAEL imesema kuwa inafanya kila lina-lowezekana – kwa kutumia mbinu za kivita na kikachero, kuhakikisha inamuua kiongozi wa kidini wa Iran, Ayatollah Ali Khamenei.

Nchi hizo mbili ambazo zimekuwa kati-kata vita kwa zaidi ya wiki moja sasa, zimekuwa “zikiumizana” kwa mashambulizi makubwa ya

makombora, huku kila moja ikidai kuchakaza ardhi ya mwenzake. Israel imekuwa ikieleza kuwa kikwazo kikubwa cha kupatikana amani ni Ayatollah. Kiongozi huyo wa kidini ana msimamo mkali kuhusu nchi yake kuendelea na mipango yake ya kumiliki silaha za nyuklia. Marekani imeingia kati kwenye vita hiyo ikisaidia swahiba wake, Israel, huku wabunge wake wengi wakipinga hatua hiyo.

Habari Kuu

Rais Samia
Suluhu
Hassan

Samia akamilisha

Na Mwandishi WETU

ALIPOINGIA madarakani wengi waliingiwa woga ulioambatana na wasiwasi, iwapo kweli mwanamke anaweza kuongoza nchi.

Hofu ya wengi ilisemwa hadharani na pengine kwa kificho.

Hata baadhi ya “wakubwa” wakiwamo wanasiasa waandamizi ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) na viongozi wachache ndani ya madhehebu, walisita kuamini kuwa ataweza.

Wapo waliothubutu hata kutamani Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ivunjwe ili kuepusha nchi kuongozwa na Samia Suluhu Hassan, aliyekuwa makamu wa rais wakati kifo cha mtangulizi wake, John Pombe Magufuli kinatokea – Machi 19, 2021.

Pia, hofu hiyo ikakomazwa na kuwepo kwa janga la dunia la mlipuko wa ugonjwa wa Covid – 19, uliotikisa dunia, yakiwamo mataifa makubwa na tajiri; Marekani na China.

Lakini, miaka minne baadaye, Rais Samia Suluhu Hassan amethibitisha kuwa woga huo haukuwa na maana yoyote.

Mafanikio ya serikali aliyoongoza “yanajisema yenyewe” na kuelezea kwa ukamilifu uwezo wa kiongozi huyo kuendesha nchi.

Katika kipindi cha miaka mitano, serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Samia, imeand-

ika historia mpya katika nyanja mbalimbali za maendeleo kitaifa na kimataifa.

Kupitia uwekezaji mkubwa katika sekta za miundombinu, elimu, afya, maji, kilimo, huduma za kijamii na uhusiano wa kimataifa, Tanzania imepiga hatua kubwa kuinua ustawi wa wananchi na kuimarisha uchumi wa taifa.

Hakuna sehemu ambayo Rais Samia amelezea kwa ufasaha, ujumla na ufafanuzi wa hali ya juu kuhisiana na hilo kama kupitia hotuba yake ya kuahirisha shughuli za Bunge la 12, Ijumaa iliyopita jijini Dodoma.

Miundombinu: Msingi wa uchumi wa kisasa

Mtangulizi wake, Dkt. John Magufuli alianzisha miradi mikubwa na miundombinu, ikiwemo ujenzi wa bwawa la kufua umeme la Julius Nyerere, mradi wa treni ya kisasa (SGR) na mradi wa daraja katika Ziwa Victoria kwa kuta-ja michache.

Alipofariki Rais Magufuli, wengi wakajiuliza iwapo anayemfuatia angeweza kutekeleza miradi hiyo, kwani ilihitaji fedha nyingi ambazo nchi haikuwa na uhakika wa kuzipata wakati huo dunia ikihangaika na mlipuko wa Covid-19.

Rais Samia kuthibitisha kuwa wanawake wanaweza, ametekeleza miradi ya bwawa la Julius Nyerere, daraja la Ziwa Victoria na kuanza kazi kwa SGR – kutoka Dar es Salaam hadi Dodoma.

Katika kutekeleza mradi wa ujenzi wa SGR, ambao unaendelea kwa kasi ya kuridhisha, vipande vya Mwanza-Isaka, Makutupora-Tabora, na Tabora-Kigoma, vinaendelea kujengwa kwa kasi.

Aidha, serikali imenunua mabehewa mapya ya abiria na mizigo na kukarabati reli za zamani (MGR).

Sambamba na miundombinu hiyo, Rais Samia anaendelea kusimamia upanuzi na uimarishaji wa bandari nchini.

Kama sehemu ya jitihada za kuimarisha bandari, serikali iliingia mkataba wa uendeshaji wa Bandari ya Dar es Salaam na kampuni ya DP World, inayosifika duniani kwa ufanisi wa kazi hiyo na faida zimeanda kurekodiwa muda mfupi baada ya kuanza kazi.

Takwimu zinaonyesha kuwa tangu kuingia kwa kampuni hiyo, ufanisi wa Bandari ya Dar es Salaam umeongezeka kwa kiasi kikubwa.

Inaendelea Uk. 7

Samia akamilisha

Inatoka Uk. 6

Pia kumekuwa na uimarishaji wa viwanja vya ndege na barabara nchini na kuchochea au kufungua fursa mpya za kiuchumi.

Kwa mfano, urefu wa barabara za lami umeongezeka kutoka kilomita 38,086.95 mwaka 2020 hadi 40,902.34 mwaka 2025, na barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 hadi zaidi ya 44,000.

Madaraja ya Tanzanite, Wami, Mpwapwa, Gereza na Daraja la Dkt. John Magufuli (Kigongo-Busisi) yamekamiliwa, yakiwa na mchango mkubwa katika kuunganisha mikoa na kuchochea biashara, hivyo kukuza uchumi.

Katika sekta ya anga, serikali imenunua ndege mpya saba kupitia ATCL, ikijumuisha ndege ya mizigo.

Ujenzi wa viwanja vya ndege ikiwamo Msalato, Dodoma; Tabora, Kigoma na Musoma, Mara unaendelea, hali inayoimarisha usafiri wa ndani na wa kimataifa.

Nishati: Umeme kwa uhakika, endelevu

Serikali imeongeza uwezo wa kuzalisha umeme kutoka megawati 1,601 mwaka 2020 hadi megawati 4,031.

Kwa kiasi kikubwa, ongezeko hilo limechangiwa na Mradi wa Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) unaozalisha megawati 2,115.

Mikoa ya Kigoma na Katavi sasa imeunganishwa na Gridi ya Taifa kwa mara ya kwanza katika historia.

Aidha, upanuzi wa vituo vya usambazaji vikiwamo Kimara, Dar es Salaam; Kisarawe na

Soga, Pwani, umeongeza uhakika wa nishati katika maeneo ya mijini na viwandani, hivyo kukuza uzalishaji na kuimarisha maisha ya wananchi.

Maji: Upatikanaji wa huduma kwa wote

Serikali imefanikiwa kutekeleza miradi 2,331 ya maji nchini kote, ikiwa ni pamoja na miradi mikubwa ya Arusha, Same-Mwanga-Korogwe, na mradi wa maji safi kutoka Ziwa Victoria unaohudumia zaidi ya watu milioni saba.

Upatikanaji wa huduma za maji safi mijini umefikia asilimia 91.6 na vijijini asilimia 85, hivyo kupunguza adha ya wananchi kusafiri umbali mrefu kutafuta maji.

Serikali pia imeanzisha mamlaka 13 mpya za usambazaji maji na usafi wa mazingira ili kuongeza ufanisi wa huduma.

Elimu: Kujenga taifa la maarifa

Katika kipindi cha miaka mitano iliyo pia, serikali imeongeza bajeti ya elimu kutoka Shilingi trilioni 4.72 hadi trilioni 6.16.

Shule mpya za sekondari, shule za sayansi za wasichana kila mkoa, shule za amali na vyuo vya VETA vimejengwa.

Pia, vyumba vya madarasa vimeongezeka hadi kufikia 254,393 nchi nzima.

Katika elimu ya juu, mikopo imeongezeka kwa wanafunzi zaidi ya 248,000 na bajeti kufikia shilingi bilioni 787.4.

Zaidi sana, mpango wa Samia Scholarship umeanzishwa kusaidia wanafunzi wa masomo ya sayansi na afya.

Afya: Huduma zasogea kwa wananchi

Idadi ya vituo vya kutolea huduma za afya imeongezeka kutoka 8,783 hadi 12,846 ndani ya miaka mitano.

Hii imesaidia Watanzania wengi zaidi kupata huduma ndani ya umbali wa kilomita tano.

Hospitali mpya za mikoa, vituo vya afya na zahanati vimejengwa na kuboreshwa.

Huduma za kibingwa ikiwamo upasuaji wa moyo, ubongo na figo sasa zinapatikana ndani ya nchi, hivyo kupunguza gharama kwa wagonjwa waliokuwa wakisafirishwa nje.

Serikali pia imeongeza bajeti ya ununuzi wa dawa, vifaa na chanjo kutoka Shilingi bilioni 276 hadi bilioni 474.



Habari Kuu**Samia akamilisha****Inatoka Uk. 7****Kilimo: Uzalishaji, usalama wa chakula**

Sekta ya kilimo imepata ongezeko la bajeti kwa zaidi ya asilimia 300, kufikia shilingi trilioni 1.24.

Upatikanaji wa mbegu bora umeongezeka kutoka tani 50,747 hadi tani 72,032, na mbolea kutoka tani 678,017 hadi tani milioni 1.21.

Tija imeongezeka kwa mazao ya chakula na nchi ina utoshelevu wa chakula kwa asilimia 128.

Serikali imejenga maghala na vihenge kwa ajili ya kuhifadhi mazao na kupunguza upotevu baada ya mavuno.

Kwa upande wa umwagiliaji, eneo linalomwagiliwa limeongezeka hadi hekta 983,466, huku serikali ikipanga kuanzisha Gridi ya Taifa ya Umwagiliaji kwa kutumia maji ya Ziwa Victoria na Tanganyika.

Uvuvi na Mifugo

Serikali imeimarisha sekta ya uvuvi kwa ku-

toa boti 160, kuwezesha vizimba zaidi ya 1,600, na kutoa ajira zaidi ya 13,000.

Ujenzi wa Mradi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko umefikia asilimia 81.9 na unatarajiwa kutoa ajira zaidi ya 30,000.

Katika sekta ya mifugo, mauzo ya nyama nje yameongezeka kutoka tani 1,774 hadi 14,701 na thamani yake kufikia dola milioni 61.

Serikali imeanzisha kampeni ya kitaifa ya chanjo na utambuzi wa mifugo, na kutoa ruzuku kwa hereni na chanjo.

Hifadhi ya jamii

Kwa kuzingatia umuhimu wa usawa wa kijamii, serikali imepanua wigo wa wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii hadi kufikia milioni 1.7.

Pensheni ya chini kwa wastaafu imeongezeka kutoka Sshilingi 100,000 hadi 150,000.

Pia, Serikali inaendelea na malipo ya pensheni kwa wazee wasio na kipato kupitia mpango wa ustawi wa jamii.

Tehama, utawala bora

Serikali imefanikiwa kutekeleza mfumo wa anwani za makazi nchi nzima, na taarifa zaidi ya milioni 12 zimeingizwa.

Tanzania imetajwa na Benki ya Dunia kuongoza Afrika Mashariki katika matumizi ya Tehama serikalini.

Hili limeongeza ufanisi, uwazi na uwajibikaji katika taasisi za umma.

Dira ya Maendeleo na mustakabali wa taifa

Kama ilivyowasilishwa na Rais Samia, mafanikio haya yanatokana na usimamizi wa kisera, utekelezaji madhubuti wa miradi ya maendeleo na ushirikiano kati ya Serikali, sekta binafsi na wananchi.

Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2050 ambayo itazinduliwa Julai 2025 inalenga kuchochea ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu, kuhakikisha Tanzania inakuwa nchi ya viwanda yenye ustawi wa watu wake.

Rais Samia anasema kuzingatia hatua zilizopigwa, nchi ipo kwenye mwelekeo sahihi kuelekea mafanikio ya kijamii na kiuchumi.

“Serikali inayoendelea ya awamu ya sita imeonesha kuwa mageuzi yanawezekana, na maendeleo yanaweza kuwa ya watu wote, siyo ya wachache,” amesema.

Olengurumwa atamani kuwepo KUB



Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa

Na Mwandishi WETU

MRATIBU wa Kitaifa wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), Onesmo Olengurumwa ameshauri Uchaguzi Mkuu 2025, uwe huru na haki ili wabunge wengi wa vyama vya upinzani wapatikane na baadaye kuwepo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni (KUB).

Amesema zamani Bunge lililokuwa na KUB, faida zilionekana ikiwepo kuwajibisha na kusi-mamia serikali ipasavyo.

Olengurumwa ametoa kauli hiyo siku moja baada ya Rais Samia Suluhu Hassan kuhutubia

na kuhitimisha shughuli za bunge, Ijumaa iliyopita - Juni 28.

“Bunge hili la 12 halikuwa na KUB, hivyo suala la uwajibikaji na kuisimamia serikali ilionekana kulegalega kutokana na muundo wake ambao ulikuwa wa chama kimoja...”

“Kwa mujibu wa Katiba tunapaswa kuwa na KUB. Maombi na matamania yangu ni uchaguzi wa Oktoba uwe huru na haki ili tupate wabunge wengi wa upinzani na baadaye tuwe na KUB...”

“Tukiwa na KUB ule ubora wa bunge utaimarika zaidi, tusirudi kwenye bunge tena bila kuwa na KUB,” alisema Olengurumwa.

Alikumbushia Bunge la 10 na 11 ambalo lilikuwa na KUB, namna kamati za bunge kama ya ile ya kudumu ya kufuatilia hesabu za serikali - PAC, zilivyokuwa na mambo ya msingi ya kuiwajibisha serikali.

“Natamani bunge lile la wakati wa kina Zitto Kabwe akiwa Mwenyekiti wa PAC na wengine, namna walivyochachafya bunge, ilisaidia mambo mengi sana ya msingi,” alisema.

Akizungumzia hotuba ya Rais Samia wakati akihitimisha bunge, alisema mengi aliyozungumza mkuu huyo wa nchi ni kweli mambo makubwa ya maendeleo yametekelezwa.

“Miradi mikubwa ya kimaendeleo imekamilika, leo tunatembea na SGR saa tatu tu tuko Dodoma kutola Dar es Salaam...”

“Miundombinu ambayo awamu ya tano ilianzisha, sehemu kubwa imekamilika na mipya imeanzishwa hilo ni jambo ambalo kama taifa lazima tuseme tu kwamba tumepiga hatua ingawa hatujakamilika na bado tuma safari ndefu kimaendeleo, lakini hatua imepigwa,” alisema.

Alisema pamoja na kwamba kuna baadhi ya sheria zimeboreshwa, lakini bado hazijatosheleza, hivyo Watanzania waendeleo kudai mabore-sho zaidi.

“Lakini tukiwa na katiba mpya ndiyo italeti hayo matamania ya maboresho ya uhakika. Nashukuru kwamba Rais Samia ametamka kuwa baada ya uchaguzi ikitokea ameshinda, tutapata katiba mpya hilo ni jambo la faraja sana,” alisema Olengurumwa.

Tafakuri ya BagonzaNa Dkt. Benson
BAGONZA

Hili la Zambia kama siyo funzo, ni kengele

RAIS (mstaafu) wa sita wa Zambia, Edgar Lungu, amefariki Juni 5, 2025 akiwa matibabu huko Afrika Kusini.

Ilipangwa azikwe nchini Afrika Kusini baada ya siku 20, yaani Juni 25, 2025 na kwamba misa ya maziko yake ingeongozwa na Askofu Mkuu wa Lusaka, Alick Banda.

Baada ya kusikika kwa taarifa hizi, Serikali ya Zambia ikafungua kesi ya kuzuia Rais Lungu kuzikwa Afrika Kusini.

Rais wa saba, Hekainde Hichilema (HH) ndiye yuko madarakani. Familia ya Lungu imekataa kukubaliana na serikali kuhusu taratibu za mazishi kwa kusema marehemu aliacha wosia kuwa akifa, Rais Hichilema asisogelele wala kuhudhuria mazishi yake.

Alipokuwa madarakani, Rais Lungu alimweka korokoroni rais wa sasa – HH, mara 15 kwa tuhuma mbalimbali.

Naye Rais Hichilema alipomshinda Lungu na kuingia madarakani, akamuweka kwenye kifungo cha ndani na kumnyima uhuru wa kutembea, kwenda kanisani na hata kugombea katika uchaguzi mkuu ujao mwaka 2026.

Yote haya yanatia aibu pande zote, lakini kwetu Tanzania, haya kama siyo mafunzo kwetu, basi ni kengele ya kutuamsha tuweke mambo yetu vizuri.

Yapasa kuelewa kuwa wale tulio madarakani kama mimi, tujue ipo siku madaraka haya yataondoka, kwa njia nzuri au mbaya. Kutambua tu kuwa yataondoka, kutufanye kunyenyekea na kutenda wema na haki.

Yatupasa kuelewa kuwa wale wanaotafuta madaraka, ni vyema kutambua kuwa “mapenzi ya kuposea, siyo ya kuolea na kutunza ndoa.”

Ni rahisi kulalamika kuliko kulalamikiwa. Mkiingia madarakani msitumie sheria mbaya zilizoachwa na watangulizi wenu kuwatesa wapinzani wenu wa kisiasa. Unyenyekevu si udhai-fu, bali unahifadhi nguvu na raslimali.

Kwamba ukiwa madarakani, una uwezo wote wa kukataa ushauri unaopewa, lakini, huna uwezo wala madaraka ya kukataa madhara ya ukaidi wako wa kukataa ushauri.

Machozi yako wakati wa majuto ni kama yale ya samaki. Utazomewa hata na uliowasaidia. Nimeyaona kwa Lungu.

Kwamba kila aliye madarakani hutoa hotuba nzuri na maelekezo sahihi. Hotuba za Hichilema ni tamu na zinavutia, lakini zinaficha wingi wa kisasi na uchungu. Wasaidizi hawasilizi hotuba zake; wanakumbuka aliyotendewa.

Kiongozi mzuri ni mwenye uwezo wa kudhibiti chawa wake.


Kwamba familia za viongozi humwangusha kiongozi kabla hajaangushwa na wapinzani wake. Kiongozi anayelaumiwa na familia yake kwa “kutowasaidia”, anaweza kuwa kiongozi bora kuliko “anayebeba” familia nzima.

Kiongozi “akiwasahau” ndugu zake, anakuwa amewaepusha na mateso baada ya yeye kuondoka. “Akiwabeba” anaondoka na kuzama nao. Nimeliona kwa Lungu.

Kwamba madaraka makubwa mikononi mwa mtu mmoja, ni hatari kwake, marafiki na adui zake. Kwa kuwa ndugu na marafiki hawana kinga, ni hekima wakijitenga na mwenye madaraka.

Kipimo halisi cha maadili ya mwenye madaraka makubwa, ni pale hata maadui na wapinzani wake wanapojiona wako salama mikononi mwake. Yaani adui yako usimwonee wala kumpendelea.

Mwandishi wa safu hii ni Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Jimbo la Karagwe. Ni mchangiaji maalum wa safu na makala ndani ya Pambazuko.



RAIS mstaafu wa
sita wa Zambia,
Edgar Lungu,

Na Godwin CHILEWA,
Houston



Kurunzi la Intelejensia

Chanya, hasi hotuba ya Samia bungeni



JUNI 27, 2025 - Rais Samia Suluhu Hassan, alihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ikiwa ni kazi yake ya mwisho kulihitimiza.

Katika hotuba yake, Rais Samia alizungumzia masuala muhimu ya kitaifa ikiwa ni pamoja na hali ya uchumi, siasa, ulinzi na usalama, pamoja na maandalizi ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2025.

Hotuba ya Rais Samia ilipokelewa vyema na wabunge waliohudhuria kikao ambao walimshangilia kumpongeza mara kwa mara wakati akieleza mafanikio ya uongozi wake, kutoa mwelekeo wa taifa, na msimamo wake binafsi.

Hata hivyo, kwa wananchi wengine – ambao wameweka mawazo yao kwenye mitandao ya kijamii, hotuba hiyo ilionekana kuwa imejaa maelezo yasiyobeba maisha halisi ya Mtanzania sasa - wa kawaida.

Katika hali ya kawaida ni rahisi kusema kwamba wanaohoji ukweli au uhalali wa hotuba ya Rais Samia ni wapinzani, au wachokonozi wasio na jema, waliotayari kupinga na kukosoa kila linalosemwa na rais, hata hivyo kuna haja ya kutafakari na kuiweka hotuba hiyo kwenye mizani ili kupata majibu japo ya kujiridhisha tu.

Rais Samia alilieleza Bunge kuwa uchumi wa taifa unaendelea kukua, akitaja ukuaji wa Pato la Taifa (GDP), mfumuko wa bei kuwa wa chini, na uwekezaji kuongezeka. Hata hivyo, hoja hii

inapingwa vikali na uhalisia wa maisha mitaani.

Kwa ujumla, bei ya bidhaa muhimu kama unga, mafuta, na sukari imekuwa ikipanda kila mwaka.

Mfumuko wa bei wa kitaalamu unaweza kuonekana mdogo kwenye takwimu, lakini mfumuko wa bei halisi katika maisha ya kila siku, ni mkubwa mno.

Wananchi wanahaha, na wengi wanakula mlo mmoja kwa siku. Kimsingi, uchumi unakua kwenye takwimu zaidi.

Ukosefu wa ajira kwa vijana unazidi kuwa janga la kitaifa. Takwimu za ajira zilizotajwa hazioneshi ajira zenye staha na kipato cha kumtoshia Mtanzania.

Serikali imekuwa ikisisitiza kuhusu kujiajiri bila kujali vijana hawana mitaji wala elimu mahususi ya biashara.

Kupanda kwa gharama za maisha, huku mishahara ya wafanyakazi wa umma na sekta binafsi ikiwa haijaongezwa kwa muda mrefu, kunafanya mafanikio ya uchumi yaonekane ya “kitabaki” — yaani mafanikio ya vitabuni, siyo ya uhalisia au vitendo.

Kumbe ni muhimu sana serikali iwe na sera za kweli za kukuza kipato cha mwananchi mmoja mmoja, siyo kuonyesha ukuaji wa juu usiojidhihirisha kwa walalahoi.

Akizungumzia siasa, Rais Samia ameonesha umahiri wa kutoa uimara wa demokrasia bila kuzungumza namna uhalisia kwenye vyama vya siasa, ambako viongozi wa upinzani wanaendelea kufuatiliwa, kuzuiwa kufanya mikutano, kufunguliwa mashitaka, au kubughudhiwa na vyombo vya dola.

Chama kikuu cha upinzani, Chadema kimekuwa kikihujumiwa kwa kila hali kwa lengo la kukidhoofisha au kukiua kabisa.

Siyo hivyo tu, sheria kadhaa zinazoonekana kuwa kandamizi ikiwamo Sheria ya Huduma za Habari, Sheria ya Makosa ya Mtandao, na baadhi ya vifungu kandamizi vya Katiba, bado vinaendelea kutumika kuwakandamiza wanaharakati, waandishi wa habari, na raia wanaokosoa serikali.

Kurunzi la Intelejensia**Chanya, hasi...****Inatoka Uk. 11**

Rais alizungumzia maridhiano ya kisiasa, lakini hakuna mchakato wa kitaifa wa maridhiano unaoendelea kwa uwazi au kwa kushirikisha wadau wote wa siasa.

Kumbe ni vyema badala ya kuzungumzia maridhiano kwa maneno matamu, serikali ichukue hatua madhubuti za kisheria na kisera, kulinda demokrasia, uhuru wa habari, na siasa shirikishi.

Wanasiasa na wanaharakati waliowekwa mahabusu waachiliwe na kupewa haki na uhuru wa kweli kufanya shughuli zao kwa mujibu wa sheria.

Akizungumzia ulinzi na usalama, Rais Samia alisisitiza kuwa Tanzania ni nchi salama na yenye amani. Hili ni jambo la kupongezwa, lakini lina sura nyingine iliyo tata.

Ripoti kutoka kwa mashirika huru ya ndani na nje ya nchi zimeonyesha matumizi ya nguvu kupita kiasi dhidi ya waandamanaji, kukamatwa holela kwa raia, na ukandamizaji wa wanaharakati wa haki za binadamu.

Lipo pia lile suala tata la utekaji nyara na kupotea kwa watu kwa namna ya ajabu, au kuuawa na watu wasiojulikana, ingawa hapa alielekeza Jeshi la Polisi kuhakikisha mambo haya yanakomeshwa.

Baadhi ya watu wamehoji uhalisia wa kauli hiyo kwa kuzingatia baadhi ya watu waliokuwa wakihoji suala la kupotea kwa watu walionekana ni wasaliti na kushughulikiwa.

Hakuna asiyejua kwamba amani ya kweli haijengwi kwa kukandamiza kelele za wananchi, bali kwa kusikiliza kilio chao. Kumbe ni muhimu serikali itengeneze mazingira ya usalama wa kweli kwa raia wote—usalama wa maisha, mali, na uhuru wa kujieleza.

Kuwapa silaha za kisasa na mafunzo bora polisi ni muhimu sana, lakini hilo siyo suluhisho la amani, bali ni kuwasha moto wa hofu.

Amani huja wananchi wanapotii sheria bila shuruti kwa sababu wana imani na uongozi wao, na matumbo yao 'hayaungurumi' kwa njaa.

Akizungumzia Uchaguzi Mkuu 2025, Rais Samia aliahidi kuwa utakuwa huru na wa haki.

akuna asiyejua kwamba amani ya kweli haijengwi kwa kukandamiza kelele za wananchi, bali kwa kusikiliza kilio chao. Kumbe ni muhimu serikali itengeneze mazingira ya usalama wa kweli kwa raia wote—usalama wa maisha, mali, na uhuru wa kujieleza.

Hii ni kauli nzuri, lakini inafifia bila kuwepo kwa mabadiliko ya kweli.

Kimsingi, inayoitwa Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi bado haijapata mabadiliko makubwa ya kisheria ili iwe huru kweli, isipokuwa kubadilishwa jina.

Mfumo wa kuhesabu na kutangaza matokeo haujawekewa njia huru ya uthibitishaji. Usimamizi wa uchaguzi unategemea sana vyombo vya dola vinavyotuhumiwa kwa upendeleo.

Na hata wasimamizi wa uchaguzi katika majimbo, ni wateule wa Rais wa Tanzania, ambaye ni mgombea, na mwenyekiti wa chama tawala.

Kumbe kuna haja ya kuanza haraka mchakato wa mageuzi ya uchaguzi kwa kushirikisha vyama vya siasa, asasi za kiraia, na wananchi. Hili ni jambo la msingi. Bila hivyo, uchaguzi wa 2025 utakuwa ni kivuli cha demokrasia.

Wananchi wengi wanaona hotuba ya Rais Samia ni sehemu ya kampeni ya awali kwa uchaguzi ujao. Kwa kutumia jukwaa la Bunge, Rais alitoa taswira ya taifa linalong'aa, bila kuonesha kuwepo kwa majeraha.

Ni vyema kukumbuka kwamba Tanzania ni nchi yenye watu wengi werevu, wavumilivu, na wenye matumaini, lakini matumaini haya yana-hitaji ukweli.

Hotuba ya Rais Samia ilipaswa kuwa nafasi ya kuonesha hali halisi, kukiri changamoto, na kueleza mipango ya kweli ya kuzitatua.

Ni ukweli usiopingika kwamba hakuna mtu asiyeifanya makosa. Ni kwa sababu hii mtu anayetambua makosa yake, kuyakiri na kuyasahihi-sha hujipatia heshima na ridhaa ya watu kuliko anayetumia ujanja kuficha.

Wakati umefika sasa kwa serikali kujipima kwa mambo halisi na kuyasema hadharani na penye changamoto au makosa, basi yasemwe hadharani na kuyaombea msamaha ili kujenga Tanzania yenye neema na baraka tele.

Na Dkt. Hellen Kijo
BISIMBA



Kona ya Dkt. Bisimba

Yapi mafanikio Bunge la 12?

JUNI 27, 2025 - Rais Samia Suluhu Hassan alitoa hotuba ya kuhitimisha shughuli za Bunge la 12.

Katika hotuba hiyo, alieleza kuwa atalivunuja rasmi Bunge hilo mnamo Agosti 3, mwaka huu.

Bunge hili lilianza rasmi kwa kufunguliwa na Rais Dkt. John Magufuli Novemba 2020 – akiwa kiongozi wa awamu ya tano ambaye kwa sasa ni marehemu.

Bunge hili la 12, limekuwa na wabunge wachache sana wa upinzani kiasi cha kutokuwa na kiongozi wa kambi rasmi ya upinzani, bali kuwa na kambi ya walio wachache.

Lilipoanza lilikuwa katika mwendelezo wa kutokuwa na matangazo ya Bunge ya moja kwa moja (mubashara) yaliyozuliwa tangu Bunge la 11.

Ilikuwa heri pale Aprili 4, 2022, wakati matangazo ya moja kwa moja yaliporejeshwa tena kwa tangazo la spika.

Inavyoonekana, mvuto wa kufuatilia bunge ulishapungua na machache niliyofuatilia hayakutoa nguvu ya kufuatilia kama ilivyokuwa huko nyuma wakati bunge likionekana kuisimamia serikali na kuibua masuala yaliyokuwa na tija kwa wananchi.

Bunge hili katika suala la mkataba wa ubin-afsishaji wa Bandari za Tanzania Bara, halikuwa na sauti moja na wananchi walio wengi ambao waliona mkataba ule usingekuwa na manufaa kwa Watanzania.

Bunge lilianza na Spika Job Ndugai, alipojiuzulu alipokea Spika Tulia Ackson, akiwa ni mwanamke wa pili kuwa spika baada ya Anne Makinda.

Pia Bunge lilipata Katibu wa Bunge wa kwanza mwanamke, Nene Mwihi, jambo lililozidisha sifa kwa Tanzania kuwa na ongezeko la usawa wa kijinsia katika nafasi za juu.

Mihimili miwili yenye wanawake na mhimili mmoja wenye mwanamke na katibu wake. Sifa hii maana yake kwetu ni ipi?

Tukijitazamisha kwenye kazi kuu za bunge ambayo ni wawakilishi wa wananchi, tunajiuliza katika maswali 5,259 na 18,075 ya nyongeza yaliyo-ulizwa na wabunge na yale 253 ya papo kwa papo



kwa waziri mkuu, mangapi yalitokana na uwakilishi?

Kwamba ni wabunge wangapi walikutana na wananchi wa jimboni kwake au waliwasiliana nao wakaeleza yanayowakabili nao wakachukua jukumu la kuuliza serikali kutoa majibu na ni majibu mangapi ambayo wananchi waliyapokea kwa kuridhika?

Mengine huyaweza kuwa ni maswali yaliyotokana na hali halisi iliyo wazi ambayo mbunge aliona serikali ilipaswa kufanya jambo, lakini haikufanya na hivyo anauliza swali na akiamini hata anaowawakilisha swali hilo likijibiwa, litakuwa na manufaa kwao.

Katika maazimio 19 wabunge waliyopitisha, manne yalikuwa ya kupongeza na walimpongeza Rais Samia kwa utendaji wake mzuri.

Katika hayo, pia swali linabaki palepale. Wale wabunge waliokuwa wakitaka wageni waliokataliwa kuingia nchini – kutoka Kenya na Uganda, wateswe kabla ya kurudishwa makwao, walipata muongozo kutoka wapi?

Katika Bunge hili kuna wakati mbunge alipendekeza ijadiliwe hoja ya watu wanaosemekana kutekwa na waliopotea hata kuuawa, lakini suala hili halikukubaliwa na spika na halikujadiliwa kabisa pamoja na kuwa limekuwa ni suala tete.

Hadi sasa Bunge linapovunjwa jibu kuhusu suala hilo halijapatika kutoka kwa hawa wawakilishi ambao wanarejea kuja kuomba tena uwakilishi.

Bunge hili la 12 lilipoanza, Mahakama ya Rufaa Tanzania, ilikuwa imetoa uamuzi wa kulitaka lire-kebishe Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 - kifungu cha 13 na cha 17, vinavyokiuka haki ya mtoto wa kike, lakini hadi linavunjwa jambo hilo halijafanyika.

Katika mafanikio ya bunge hili, ni yapi ambayo kwa hakika Mtanzania akiyasikia atagonga tano?

Mwandishi wa safu hii ya kila wiki, ni mwanaharakati wa demokrasia, haki za binadamu na mwanazuoni wa falsafa ya sheria. Anapatikana kwa namba 0713 337 240.

Habari**Bangi ya Malawi...****Inatoka Uk. 4**

Mwaka 2023, walioamua kulima – kwa kuunganisha mitaji na wenyeji, walifanikiwa kupata fedha nyingi kwa kuwa kilimo kililipa zaidi, hasa baada ya kuwepo kwa ushindani kutoka kampuni za kununua zao hilo.

Pambazuko limedokezwa kuwa baada ya mafanikio hayo, Watanzania hao na wengine wapya, waliongeza mitaji yao ili kupata zaidi kwa msimu uliokuwa unafuata, mwaka jana – 2024.

Kumbe bahati haikuwa upande wao, kwani, licha ya kuwa na mavuno makubwa, kampuni za kununua bangi ama zilisimamisha biashara hiyo, au ziliacha kabisa na kuondoa mitaji yao nchini Malawi.

Kwanini kampuni zimesimama?

Kampuni moja kubwa ya Marekani iliyokuwa ikinunua bangi kutoka Malawi, USCA, mwaka jana ilisimamisha shughuli zake bila kueleza sababu za msingi.

Kusimama kwa kampuni hiyo iliyokuwa ikinunua bangi kwa wingi, kumeumiza wakulima wengi na hata wachuuzi wa kati ambao walikuwa wakinunua kutoka kwa wakulima na kuuza.

Kampuni nyingine kubwa ya ununuzi wa bangi ya Malawi, Invegrow, nayo, bila kueleza sababu, ilipunguza kiasi cha kununua zao hilo, hivyo kuchangia kudorora kwa biashara hiyo.

Tangu mwaka jana, kiasi kikubwa cha bangi kimehifadhiwa kwenye maghala huku walio-wekeza wakishindwa kupata suluhisho la hatma ya “mzigo” mkubwa walionao.

Bei ya bangi Malawi

Tangu mwaka 2022, bei ya kilo ya bangi nchini Malawi ilikuwa ikinunuliwa kati ya Shilingi 215,000 hadi 395,000 kwa kilo moja, kutegemea na ubora wa zao lenyewe.

Hata hivyo, bei kutoka kwa wakulima moja kwa moja ilikuwa chini ya hapo, ingawa uchunguzi umebaini kuwa ilikuwa vigumu sana kwa wakulima kuuza moja kwa moja kwenye kampuni bila kupita kwa madalali.

Tanzania yazungumza

Akizungumza na Pambazuko jijini Dodoma hivi karibuni, Kamishna wa Mamlaka ya Dawa

za Kulevya (DCEA), Aretas Lyimo, alithibitisha kuwa wapo Watanzania ambao “wamelizwa” kwenye biashara hiyo.

Akisimulia, Lyimo alisema baada ya Malawi kuruhusu kilimo cha bangi, watu kadhaa nchini waliiona kuwa hiyo ni fursa.

“Watu wakatoka hapa kwenda Malawi ili kulima bangi, lakini ilipofika wakati wa mavuno hakukuwa na soko la bidhaa hiyo na kusababisha wapate hasara kubwa,” anasema.

Lyimo alisema yupo mfanyabiashara mmoja ambaye alikopa shilingi milioni 300 benki kwa ajili ya kwenda kuwekeza kwenye kilimo hicho na fedha hizo zote zimetumbukia shimoni.

“Hivi sasa yule bwana yupo mahututi, amepata stroke (kiharusi) na deni la benki bado lipo,” Lyimo ameliamba Pambazuko.

Lyimo anasema Watanzania hao waliamua kukimbilia Malawi kulima bangi baada ya Tanzania kusimamia msimamo wa kutoruhusu kilimo cha zao hilo ambalo kwa mujibu wa sheria ni sehemu ya dawa za kulevya.

“Tumekuwa tukipokea maombi mengi ya Watanzania wanaotaka waruhusiwe kulima bangi. Wamekuwa wakishawishi hivyo baada ya nchi kadhaa, zikiwemo za jirani, kuruhusu kilimo cha bangi,” anafafanua Lyimo.

Madhara kwa Tanzania

Lyimo anasema hata ruhusa ya kulima bangi iliyowekwa na Malawi, imesababisha matatizo kwa nchi jirani ikiwemo Tanzania.


Akifafanua, Lyimo anasema baada ya zao hilo kukosa soko, wafanyabisahara hao walibuni mbinu ya kuisindika bangi hiyo kienyeji na kuzalisha ‘skanka’ ambayo kwa kiasi fulani imekuwa ikiingizwa nchini kinyemela.

“Utaona katika ripoti yetu ya hali ya dawa za kulevya kwa mwaka 2024, tumeleza kukamatwa kwa kiasi kikubwa cha skanka...”

“Sehemu kubwa ya skanka hii inaingizwa nchini kutoka nchi jirani ambako bangi inaruhusiwa kulimwa...”

“Kwa kuwa bangi hiyo imekosa soko, basi wale wafanyabiashara wanatafuta namna ya kupunguza hasara wanayopata kwa kuisindika bangi hiyo na kuzalisha skanka ambayo wanaisafirisha katika nchi zetu,” anasema.

Yaliyojiri ‘lalasalama’ bungeni



Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma

Na Mwandishi WETU, Dodoma

BUNGE la 12 la limehitimisha vikao vyake rasmi mjini Dodoma mwishoni mwa wiki iliyopita kwa stahili ya aina yake, huku kila mbunge aliyesimama kuzungumza akiaga wananchi wake na “kujipigia debe” kwa kuomba ridhaa ya kurejeshwa bungeni.

Mtindo huo wa kuaga ulitumiwa pia na mawaziri ambao walipata nafasi ya kusimama kuchangia jambo lolote lililokuwa linajadiliwa au kuwasilisha hoja.

Wabunge hao walitumia wasaa huo wakati walipokuwa wakichangia hoja mbalimbali za serikali zilizowasilishwa bungeni hapo.

Mbunge wa Geita Vijijini (CCM), Joseph Musukuma, licha ya kuomba kura zake, pia alimpigia debe Spika Dkt. Tulia Ackson kwa kumuomba kura kwa wananchi wa jimbo jipya la Uyole, ambako tayari amechukua fomu kuomba ridhaa ya kugombea ndani ya chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM).

“Mheshimiwa Spika umefanya kazi kubwa ya kuliongoza bunge, awali wakati unatuomba kura nilijiuliza utaweza? Lakini umefanya vizuri na leo tunajivunia wewe kitaifa na kimataifa, kwani pamoja na uspika wa Tanzania, lakini pia ni Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani (IPU), hongera sana...”

“Nikuombe na wewe utuombee sisi, hatuna mashaka nawe, tunawaomba wana Uyole wakupitishe, sisi tuna kazi na wewe, iwe jua iwe mvua, nakuombea sana...”

“...Nimeliweka jimbo langu kwenye ramani, nawaomba waheshimiwa mniombee niweze kurudi tena na kulisukuma gurudumu la maendeleo...”

“Wangapi mtaniombea hebu nyoosheni mikono juu,” alisema Msukuma huku akishangiliwa na wabunge.

Nao wenyeviti wa bunge walipewa wasaa kuzungumza kwa niaba ya wabunge.

Wenyeviti hao; Najma Murtaza Giga, ambaye ni Mbunge wa Viti Maalum, Deogratius Mwanyika -Mbunge wa Njombe Vijijini na Dkt. Joseph Mhagama (mbunge wa Madaba).

Walimshukuru Spika Tulia kwa kufanya nao kazi vizuri na kuwapatia mwongozo mzuri wakafanikiwa kuliendesha vyema bunge.

Akizungumza kabla ya Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, kutoa hoja ya kuahirisha Bunge, Spika Dkt. Tulia aliwashukuru wabunge kwa kufanya kazi pamoja kwa miaka mitano kwa umoja na mshikamano.

“Nikitaja hapa miaka mitano mnafahamu kwamba bunge hili lilipata kuongozwa na maspika wawili, likianziwa na mheshimiwa Job Yustino Ndugai, kisha nikapata nafasi mimi ya kupokea kijiti,” alisema Dk. Tulia kisha kushangiliwa na wabunge kwa kugonga meza.

Spika alisema kutokana na uzito wa shughuli hiyo ya Rais Samia Suluhu Hassan kuingia bungeni kulihutubia na kulivunja, alimtaka Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Bunge, William Lukuvi kutengua kanuni ili kuruhusu ugeni huo kuingia bungeni; naye akafanya hivyo.

Makala

Mbuyu wenye taswira ya Bikira Maria Saadan



Huu ndiyo mti wenye sanamu ya Bikira Maria ndani ya Hifadhi ya Taifa Saadani.

Na Arodia PETER, Bagamoyo

KWENYE kitabu Kitakatifu cha Biblia, inaelewa kwamba Mwenyezi Mungu aliumba dunia na vitu vyote vilivyomo. Na kamwe hakuwahi kukosea katika uumbaji wake.

Vitabu vya dini ya Kikristo vinamtambua Bikira Maria kuwa Mama yake Yesu Kristo na Kitabu cha Qur'an Tukufu – kwa Waislam, ikimtambua kuwa mama yake Issa bin Mariam, huku akiheshimika kuwa Mama Bora.

Maeneo mengi duniani, hasa miongoni mwa Wakristo, Bikira Maria ni mmoja wa Watakatifu wanaoheshimika sana.

Ilikukamilisha Ibadakwa Mama huyo, Wakris-

to wamekuwa wakitengeneza vitu mbalimbali ikiwa ishara ya kutegemea maombezi yake. Picha na taswira za Bikira Maria ni jambo lililozoeleka sana.

Lakini, katika kile kinachoweza kuelezwa kuwa ni maajabu, taswira ya picha ya Bikira Maria, inayofanana na sanamu ambazo hutumika na Wakristo kufanya ibada kwa Bikira huyo, imegunduliwa kwenye mti wa mbuyu uliopo katika Hifadhi ya Taifa ya Saadan wilayani Pangani, Tanga.

Taswira hiyo ambayo iligundulika mwaka 2019 ndani ya hifadhi hiyo, imetajwa kuwa ni maajabu mapya yanayoongeza upekee wa hifadhi hiyo kwa macho na masikio ya kawaida ya watalii wa ndani na nje ya Tanzania.

Taswira hiyo iliyokita katikati ya mti mkubwa wa mbuyu, inaonekana vizuri ukiwa umbali wa mita 100 mpaka 50, lakini kadri unavyousogelea mbuyu huo, ndivyo inavyopoteza mwonekano wake.

Kwa wanaofahamu sanamu ya Bikira Maria, akiwa na mavazi yake yanayoanzia kichwani na kufika chini ya miguu, ndivyo sanamu hiyo inavyoonekana kwa uwazi.

Ofisa Muhifadhi Idara ya Utalii Hifadhi ya Saadani iliyo chini ya Shirika la Hifadhi la Taifa (Tanapa), Daud Gordon, anaeleza kuwa taswira hiyo ya Bikira Maria, imekuwa kivutio kipya na inafaa kutumika kuwa nyenzo muhimu katika kukuza utalii wa kiimani na hata kuwa sehemu ya hija kwa waamini wa Kikristo hususan, wanaomheshimu Mama huyo kadiri ya mapokeo ya imani zao.

Gordon anaeleza kuwa taswira hiyo inaweza kuwapa wageni fursa ya kutafakari juu ya ukuu wa Mungu, uumbaji wake na imani wanazoshikilia, huku wakiwa katikati ya maajabu ya asili.

“Sanamu (taswira) hiyo inayoonekana katikati ya mti wa mbuyu, imeshuhudiwa na watalii mbalimbali wanaofika hapa. Hakika hili ni jambo la kipekee...”

“Siyo hadithi, bali ni uhalisia, niwaombe na kuwakariribisha Watanzania waje kujionea maajabu haya ambayo yameonekana na kutambuliwa miaka ya karibuni,” anasema Gordon.

Inaendelea Uk. 17

Makala/Habari

Mbuyu wenye taswira...

Inatoka Uk. 16

Hifadhi ya Saadani inapatikana katika mikoa ya Pwani - Wilaya ya Bagamoyo na Tanga, wilaya za Pangani na Handeni, ni pekee nchini inayopakana moja kwa moja na Bahari ya Hindi, ambapo wanyama na binadamu hukutana kwenye ufukwe wa bahari kupunga upepo na kupumzika.

Kwa mujibu wa mwongozo watalii katika eneo hilo, Fredy Nesto, taswira hiyo ya Bikira Maria iligundulika mwaka 2019, ikiwa katika mbuyu wenye zaidi ya miaka 100 na ambao historia inaonyesha ni kati ya miti ya mibuyu iliyo-tumika kunyongea watumwa.

Nesto alisema, tayari watalii kutoka maeneo mbalimbali wameanza kufika kwenye eneo hilo na kulitumia kwa maombi mbalimbali na baadhi wanarudi kueleza, kushukuru kwa mafanikio

waliyoyapata kulingana na imani zao baada ya kuufikia mbuyu huo.

Aidha, hifadhi hiyo pia inajumuisha historia mbalimbali ikiwa ni pamoja na biashara ya utumwa, makaburi saba ya wamisionari walio-kuja kueneza Ukristo katika ukanda wa Pwani wakiongozwa na Mjerumani, James Lebman ambaye alifariki Februari 28 mwaka 1882 akiwa na miaka 45.

Maeneo ya pwani mwanzoni yalitawaliwa na utawala wa kisultani ambao ulieneza dini ya Kiislam kabla ya miaka ya 1880, walipoanza kuingia wamisionari wa kijerumani ambao hata hivyo hawakufanikiwa kueneza ukristo katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa kumbukumbu zilizopo, mwili wa Lebman ulishindwa kusafirishwa kwenda kuzikwa kwao Ujerumani kutokana na ukosefu wa usafiri, kwani wakati huo hakukuwepo na ndege wala miundombinu rahisi kwa safari ya masafa.

Bangi ya Malawi...

Inatoka Uk. 14

Mafanikio makubwa

Katika taarifa ya Hali ya Dawa za Kulenya ya Mwaka 2024, DCEA inaonyesha kuwa kume-kuwa na mafanikio katika kudhibiti dawa aina ya cocaine.

Kamishina wa Tiba na Kinga wa DCEA, Dkt. Peter Mfisi aliliambia Pambazuko kuwa hali hiyo inatokana na kukamatwa kwa mtu ambaye ndiye alikuwa anaendesha mtandao wa biashara hiyo haramu nchini.

Anasema kukamatwa kwa mtu huyo kume-kata mtandao uliokuwa unatumika kuleta na kuzisambaza dawa hizo nchini.

Kinara huyo wa dawa za kulevya alikamatwa Jan- u- ari mwaka huu akiwa na gramu 692.336 za cocaine.

Hali ya dawa za kulevya

Taarifa hiyo ya DCEA inaonyesha kuwa bangi imeendelea kuwa kinara wa aina za dawa za kulen-

zinazozalishwa na kutumika kwa wingi nchini.

Taarifa hiyo inaonyesha kuwa katika mwaka 2024, kiasi cha tani 2,303.2 za bangi zilikamatwa nchini zikihusisha watuhumiwa 7,981 ambao kati yao wanaume walikuwa 7,475 na wanawake 506.

Kwa upande wa mirungi, taarifa hiyo inabainisha kuwa jumla ya tani 18.45 za dawa hizo zilikamatwa zikihusisha watuhumiwa 1,256 wakiwamo wanaume 1,048 na wanawake 208.

Wakati kiasi cha bangi iliyokamatwa mwaka 2024 kikiongezeka kutoka tani 1,757 zilizokamatwa mwaka 2023, kiasi cha mirungi kilichokamatwa mwaka 2024 kilipungua kutoka tani 202.74 iliyokamatwa mwaka 2023.

Athari chanya za kukamatwa kwa kinara wa biashara ya cocaine kinaonekana kupitia takwimu kwani taarifa inaeleza kuwa wakati mwaka 2023 zilikamatwa kilo 3.04 za dawa hizo za kulenya, kwa mwaka 2024 cocaine iliyokamatwa ilipungua hadi chini ya kilo moja yaani gramu 850 pekee.

Hata kiasi cha heroin kilichokamatwa nacho kimepungua kutoka kilo 1,314 mwaka 2023 hadi kilo 433.16 mwaka 2024.





Uchumi & Biashara

Serikali kuimarisha usimamizi wa kodi

Na Mwandishi WETU, Dodoma

BUNGE limepitisha Muswada wa Sheria ya Fedha ambao una vipengele vinavyolenga kuwezesha serikali kuwa na usimamizi imara wa makusanyo ya kodi.

Muswada huo uliwasilishwa bungeni na Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, mara baada ya Bunge kupitisha bajeti kuu ya mwaka 2025/26.

Muswada huo, ambao unatarajiwa kusainiwa na Rais Samia Suluhu Hassan kabla ya Julai Mosi mwaka huu, una vipengele vinavyoleta mageuzi makubwa ya kikodi kwa lengo la kukuza mapato ya ndani, kuboresha mazingira ya biashara na kufanikisha utekelezaji wa bajeti ya taifa.

“Muswada huu unapendekeza marekebisho katika sheria zaidi ya 30, na unalenga kuweka misingi ya kikodi iliyo pana, shirikishi na yenye

usawa kwa sekta zote za uchumi,” alisema Dkt. Nchemba wakati akiwasilisha muswada huo.

Katika hotuba yake bungeni Juni 25, 2025, Dkt. Nchemba alieleza kuwa muswada huu umebeba hatua kadhaa za kimkakati kwa ajili ya kuimarisha ukusanyaji wa mapato, kupunguza misamaha ya kodi isiyo na tija, na kurasimisha sekta zisizo rasmi.

Aidha, mageuzi hayo yanahusisha ongezeko la viwango vya baadhi ya kodi, kuanzisha tozo mpya, pamoja na maboresho katika mifumo ya usimamizi wa mapato.

Katika marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, serikali imependekeza kutoza kodi ya zuio ya asilimia 10 kwenye faida isiyogawiwa kwa wanahisa ndani ya miezi 12.

Hatua hii inalenga kushajiisha matumizi ya faida kwa maendeleo ya biashara na siyo kuweka akiba bila tija ya kiuchumi.

Aidha, kiasi cha hasara mlimbikizo kinachoruhusiwa kupunguza mapato katika sekta ya madini na gesi, kimepunguzwa kutoka asilimia 70 hadi 60, ikiwa ni hatua ya kuongeza mapato ya serikali na kupunguza mianya ya kukwepa kodi.

Ushuru wa bidhaa

Muswada unapendekeza kuongeza ushuru wa bidhaa katika maeneo mbalimbali kama vile bia, mvinyo na vinywaji vikali; ushuru unaongezwa kwa shilingi 10, 15 na Sh 25 kwa lita mtawalia.

Hatua hiyo inalenga kukusanya fedha kwa ajili ya kuchangia gharama za afya na Mfuko wa Bima ya Afya kwa Wote.

Ushuru mwingine umeongezwa kwenye sabuni zinazolingizwa kutoka nje mbapo sasa zitatozwa asilimia 10 ili kulinda viwanda vya ndani.

Pia, vifaa vya sigara za kielektroniki na vimuminika vyake navyo vimewekea kodi ya bidhaa kwa viwango cha asilimia 30.

Ushuru wa samani kutoka nje nao umeongezwa kutoka asilimia 20 hadi 25.

Kwenye ‘energy drinks’ serikali imeweka ushuru wa bidhaa wa shilingi 134.2 kwa kila lita utakaoanza kutumika ili kudhibiti matumizi yenye madhara kiafya na kuongeza mapato.

Muswada huo pia ulipendekeza kuondolewa kwa msamaha kwenye magazeti na lami.



Waratibu huduma za fedha wafundwa



Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji wa Fedha, Wizara ya Fedha, Dionesia Mjema

Josephine MAJURA na Chedaiwe MSUYA, Dodoma

SERIKALI imewaagiza waratibu wa biashara ya huduma ndogo za fedha kote nchini kuhakikisha wanasimamia kikamilifu utekelezaji wa sera na sheria za huduma fedha.

Lengo ni kuwabaini na kuwachukulia hatua watoa huduma wanaokiuka sheria.

Agizo hilo limetolewa na Kamishna Msaidizi wa Idara ya Uendelezaji wa Fedha, Wizara ya Fedha, Dionesia Mjema, wakati akifunga mafunzo ya kitaalamu kwa watoa huduma ndogo za fedha kutoka katika ngazi za mikoa, wilaya na halmashauri.

“Ni muhimu kila mmoja wetu awe mstari wa mbele kuhakikisha kuwa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha inatekelezwa ipasavyo, na wale wanaokiuka sheria hiyo wanachukuliwa hatua stahiki,” alisema Mjema.

Alisisitiza kuwa utekelezaji wa sheria siyo chaguo, bali ni wajibu wa kila mtoa huduma na

msimamizi wa sekta hiyo, kwa kuwa utekelezaji huo ndio msingi wa kuhakikisha uwajibikaji, uadilifu na uendeleu wa huduma ndogo za fedha katika kuwawezesha wananchi kiuchumi.

Aliwataka waratibu hao kujenga mazoea ya kuandaa na kuwasilisha taarifa za utekelezaji wa sheria hizo kila baada ya miezi mitatu, kwa mujibu wa miongozo, kwa kuwa taarifa hizo ni nyenzo muhimu katika kutathmini maendeleo, changamoto na mafanikio ya utekelezaji wa sheria katika maeneo mbalimbali ya nchi.

Pia aliwasihi waratibu hao kushirikiana kwa karibu na maofisa ushirika, wahamasishaji, wasajili, pamoja na maofisa maendeleo ya jamii, ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa sera na sheria za Huduma Ndogo za Fedha unafanyika kwa ufanisi.

Mratibu wa Biashara ya Huduma Ndogo za Fedha Mbeya, Sebastiana Mwapinga, ambaye alikuwa miongoni mwa washiriki wa mafunzo hayo, alisema kuwa mafunzo hayo ni kichocheo muhimu cha mabadiliko chanya, na kwamba wataendelea kuboresha utendaji wao hususan katika maeneo yaliyokuwa na changamoto hapo awali.

Mmoja wa wahamasishaji, Teodomila Mwenda, alisema kuwa hatua ya serikali kuwapatia mafunzo na kuwajengea uwezo wa kitaalamu siyo tu imedhihirisha dhamira yake ya dhiti ya kuimarisha sekta hiyo, bali pia imeongeza ari na motisha kwao kuendelea kutoa elimu kwa ufanisi zaidi.

Katika mafunzo hayo ya siku mbili yaliyoandaliwa na Wizara ya Fedha, taasisi mbalimbali zilipata fursa ya kutoa elimu kuhusu huduma za uwekezaji wanazotoa ikiwemo Kampuni ya Uwekezaji UTT- AMIS, Mfuko wa SELF pamoja Watumishi Housing Investment.

Jumla ya waratibu 130 wa huduma ndogo za fedha kutoka ngazi ya wizara, mikoa na halmashauri wamepatiwa mafunzo ya kitaalamu katika maeneo mbalimbali, yaliyolenga kuwaimarisha katika kusimamia na kufuatilia kwa ufanisi utoaji wa huduma ndogo za fedha katika ngazi za watoa huduma.

Kuelekea Uchaguzi 2025**BAKARI KIMWANGA****Diwani aliyefanya makubwa Kata ya Makurumla****Bakari Kimwanga****Na Elizabeth HOMBO**

MIONGONI mwa kata ambazo zimeweka rekodi ya kufanya vyema kwa kuhudumia wananchi na kuondoa baadhi ya kero, ni Makurumla iliyo-po Wilaya ya Ubungo, Dar es Salaam.

Aliyeongoza mafanikio hayo ni mwandishi wa habari na mwanasiasa, Bakari Kimwanga, aliyekuwa diwani wa kata hiyo iliyobeba sifa ya kutekeleza ilani ya chama tawala- Chama Cha Mapinduzi (CCM) katika kipindi cha miaka mitano inayoshia.

Kimwanga alipata nafasi hiyo ya kuwakilisha wananchi wa kata hiyo mwaka 2020 hadi 2025, huku akiacha historia nzuri ya uongozi wa mfano kwa kusimamia na kutekeleza miradi ya maendeleo.

Ni kutokana na jitihada zake hizo za kuwa karibu na wapigakura wake kwa miaka mitano, katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu wananchi

hao wamemwomba Kimwanga kutetea tena nafasi hiyo ili aendelee kuwatumikia.

Diwani huyo anaainisha - pamoja na mambo mengine, namna mambo mambo kumi yanayoakisi mafanikio katika kata hiyo kutokana na utumishi wake kwa umma.

Uboreshaji wa miundombinu

Kimwanga anasema amesimamia ujenzi wa barabara ya Mloka katika Mtaa wa Kilimahewa (matumizi ya fedha za jimbo kiasi shilingi milioni 7), ambayo awali ilikuwa na changamoto kubwa ya mashimo.

Anaeleza kuwa kupitia ushirikiano na Mam-laka ya Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Mbunge wa Jimbo, walifanikiwa kupata fedha na kujenga barabara hiyo, ambayo sasa inapitika kwa urahisi ingawa inasubiri utekelezaji wa mradi mkubwa wa DMDP.

Utekelezaji wa mradi wa DMDP

Anasema amehusika kikamilifu katika usimamizi na utekelezaji wa mradi wa DMDP (Dar es Salaam Metropolitan Development Project), ambao ulihusisha ujenzi wa barabara ya Mianzini-Kimamba hadi kwa Sheikh Yahaya Hussein (Kilometa 6.2) pamoja na ujenzi wa mitaro na ujenzi wa taa za barabara. Kiasi cha shilingi bilioni 18.4 zilitumika kutekeleza miradi hiyo.

“Mradi huu umeboresha miundombinu na kurahisisha usafiri kwa wakazi wa Makurumla, ambapo angalau sasa imesaidia kuiweka kata yetu kwenye ramani ya mtandao wa barabara...”

“Si hilo tu pia kupitia fedha za kila jimbo sisi tulipata kiasi cha shilingi milioni 120 ambazo zilifanya marekebisho ha barabara ya Mkasi, daraja la Mwinyi - Bucha la Vioo ikiwamo kujenga mifeji eneo la kwa Mbela - Daraja la Mwinyi,” anasema Kimwanga.

Sekta ya Elimu

Kimwanga anasema kupitia kundi la ‘ABC-Diwani Jogging Charity’, ameongoza juhudi za kuchangisha fedha kwa ajili ya ujenzi wa matundu ya vyoo katika shule za msingi ambapo kiasi cha shilingi milioni 15 zilipatikana na kusaidia kufanya ukarabati.

Pia anasema amesimamia ujenzi wa ofisi za walimu katika Shule ya Msingi Mianzini na kununua samani zake kiasi cha shilingi milioni 6.5.

Inaendelea Uk. 21

Kuelekea Uchaguzi 2025

BAKARI KIMWANGA

Inatoka Uk. 20

“Nimefanikisha pia ujenzi wa darasa moja jipya (Mianzini) kiasi cha shilingi milioni 20 pamoja na kukarabati madarasa matatu kwa ‘own source’ (mapato ya ndani) kiasi cha shilingi milioni 35...”

“Kwa upande wa Shule ya Msingi Karume, tumejenga madarasa mapya sita kwa thamani ya shilingi milioni 120 huku kwa upande wa Shule ya Msingi Dkt. Omari tumefanya ukarabati wa madarasa manane kwa mapato ya ndani kwa thamani ya shilingi milioni 45...”

“Huku shule ya Sekondari Makurumla tukijenga madarasa mapya nane kwa thamani ya shilingi milioni 160 pamoja na madawati yake,”anasema diwani huyo wa Makurumla aliyemaliza muda wake.

Kwa kutumia juhudi binafsi, Kimwanga anasema, alikuta Shule ya Msingi Mianzini inavyuka lakini kutokana na uhusiano wake mwenye na taasisi za fedha aliomba bati kwa Benki ya NMB.

“NMB wakanipatia bati 175 ambazo zimesaidia kufanya ukarabati kwa madarasa ya Mianzini pamoja na kuomba msaada binafsi Benki Kuu ambapo walitoa shilingi milioni 15 kwa ajili ya kuchimba matundu 12 ya vyoo shule ya Msingi Mianzini,”anasema Kimwanga.

Mazingira na usafi wa jamii

Kimwanga anasema amekuwa mshiriki na mhamasishaji mzuri wa usafi wa mazingira, hasa katika masoko ya Kagera na Kapera.

Pia, anasema amefanikisha mchakato wa kutafuta suluhisho la kudumu kwa Mto wa China, ambao sasa upo katika hatua nzuri ya utekelezaji wa mradi huu kupitia DMDP.

Ushirikiano wa kijamii, taasisi

Anasema amehusika katika utoaji wa msaada kwa kituo cha kulelea watoto yatima cha New Faraja Orphanage Centre, kilichopo Mtaa wa Kwa Jongo, kwa kushirikiana na taasisi maarufu ya kifedha nchini.

“Pia, katika mikutano yangu na wananchi, nimekuwa nikiwaalika wataalam kutoka taasisi mbalimbali kama; DAWASA, TANESCO, na TARURA ili kutoa majibu ya moja kwa moja na

ya kitaalamu kuhusu changamoto zinazowakabili wananchi,” anasema.

Vilevile katika kutambua nafasi ya vijana kama nguvu kazi ya taifa, Kimwanga anasema amekuwa mstari wa mbele katika kuhamasisha vijana kushiriki kikamilifu kwenye shughuli za kiuchumi.

Aidha, anasema amewezesha mikutano ya elimu na semina za ujasiriamali, hasa kwa makundi ya vijana na wanawake waliopo ndani ya kata hiyo kwa kushirikiana na CRDB pamoja na halmashauri kupitia 4/4/2.

Kupitia ofisi yake na kwa kushirikiana na maafisa maendeleo ya jamii, Kimwanga anasema amefanikisha utoaji wa elimu juu ya mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri (asilimia 4 kwa vijana, 4 wanawake, 2 walemavu).

“Vijana wengi sasa wanauelewa kuhusu furaha hizo na wameanza kujiunga kwenye vikundi vya kiuchumi vilivyosajiliwa, huku wengine wakipokea mikopo hiyo na kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi,”anasema Bakari.

Anasema juhudi hizo zimechangia kuongeza ajira binafsi, kupunguza utegemezi na kuinua kipato cha wakazi wa Makurumla, hivyo kukuza maendeleo ya kata hiyo kwa ujumla.

Huduma za afya kwa jamii

Kwa kushirikiana na Hospitali ya Ekenywa, Kimwanga anasema ameandaa programu ya “Afya Check” ambayo iliwasaidia wananchi wengi kupata tiba za kibingwa, ambayo ilitoa huduma za matibabu bure kwa wananchi wa Kata ya Makurumla na maeneo jirani.

Pamoja na mambo mengine, Kimwanga anasema programu hiyo iliwahusisha madaktari bingwa na ililenga kuwafikia wananchi zaidi ya 2,000.

Inaendelea Uk. 23



Barua za wasomaji

**Tunakaribisha barua.
Tuma kupitia**

Tuandikie kero ya eneo lako kupitia WhatsApp namba;
+255 712 792216 au tutumie kupitia email; info@
pambazuko.or.tz

**Elimu dawa za kulevya
ianzie shuleni**

Mhariri,

JUNI 23, 2025, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Sera Uratibu na Bunge, William Lukuvi, alieleza namna bangi inavyoendelea kuwa tishio katika dawa za kulevya ambazo zimekuwa ziki-kamatwa.

Waziri huyo alieleza kuwa katika kipindi cha 2024, tani 2,307.37 zilikamatwa na kati ya hizo, tani 2,303.2 ni bangi.

Ajabu ni kwamba siku hizi imekuwa kawaida kwa vijana kuvuta bangi hadharani.

Pamoja na jitihada mbalimbali za kutokomeza dawa za kulevya, lakini bangi imeendelea kushamiri huku vijana wengi ambao ni nguvu kazi ya taifa, wakiharibika.

Nadhani sasa juhudi za ziada zinahitajika kumaliza tatizo hili na kwamba elimu ianzie katika shule za msingi kuhusu madhara ya kutumia dawa za kulevya.

Amina Ally Chumbagi, Tanga.

**Misafara ya viongozi
sasa kero**

Mhariri,

Pongezi kwa kazi nzuri unayofanya wewe na timu yako ya waandishi wa habari wa gazeti la Pambazuko, hakika mnastahili maua yenu.

Napenda kupitia gazeti lako ufikishe mawazo yangu kwa wahusika ili wafikirie namna nzuri ya kukomesha kero inayokua kila siku.

Kero yenyewe ni kwamba Tanzania yetu imekuwa na viongozi wengi mno wenye kuongozwa na magari ya Polisi kila wanapokwenda ama kutoka kwenye shughuli zao.

Viongozi hawa kila wanapokaribia kupitia barabara fulani, hasa katika Jiji la Dar es Salaam, njia zote jirani hufungwa na kuzuia wananchi

**Msongamano Tegeta
unahatarisha**

Mhariri,

NAANDIKA kwa masikitiko makubwa kuelezea hali ya msongamano wa magari na watu katika eneo la Tegeta Kwa Ndevu, Kinondoni, Dar es Salaam.

Eneo la barabara hiyo ambako pia kuna stendi ya daladala, limekuwa finyu sana kiasi kwamba inakuwa vigumu kwa watembea kwa miguu kupita. Ujenzi wa barabara ya mwendokasi umezibana barabara hasa katika eneo la stendi.

Kuna malori yanayokuja kushusha bidhaa katika soko lililo karibu nayo, yanalifanya eneo la barabara kuwa dogo zaidi.

Wale wafanyabiashara waliokuwa na vibanda katika eneo la hifadhi ya barabara, ambao waliondolewa, wamerudi tena na kulifanya eneo hili kuwa hatari kwa waenda kwa miguu, kwani njia zao zote zimejengwa vibanda vya biashara.

Kifupi waenda kwa miguu katika eneo hili tunatembea roho mkononi kwani unaweza kugongwa wakati wowote; kama siyo gari, basi ni bodaboda au toyo au hata guta.

Tunaziomba mamlaka zinazohusika waliangalie suala hili kwa usalama wetu.

**John Ponera,
Mkazi wa Tegeta**

kuendelea na shughuli zao. Kibaya zaidi ni muda mrefu unaotumika kusubiri kupita kwa wakubwa hao.

Inashangaza kwamba wakubwa wanasubiriwa kupita hata kwa zaidi ya saa mbili, jambo ambalo husimamisha shughuli za maendeleo kwa muda huo.

Hii siyo sawa na inazuia mchakamchaka kukimbiza maendeleo binafsi na hata ya taifa.

Hivyo basi, endapo hakuna njia nyingine ya kukomesha kero hiyo, ni vyema serikali ikabuni njia ya kutumia helikopta au barabara mbadala ambazo zitakuwa maalum kwa wakubwa tu kuzitumia.

**Ismail Hassan, Kunduchi,
Dar es Salaam.**

Kuelekea Uchaguzi 2025



Bakari Kimwanga (kushoto), akikabidhiwa fomu ya kugombea udiwani katika ofisi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM)

BAKARI KIMWANGA

Inatoka Uk. 21

“Kwa upande wa Kituo cha Afya Makurumla ambapo sasa majengo yamekamili kwa thamani ya shilingi milioni 388 na sasa jengo la upasuaji na wodi ya wazazi itanza kutoa huduma hivi karibuni (uzinduzi umefanyika Juni 5, 2025).

“Pia tunaendelea na kufanya maboresho ya huduma za kisasa na za kibingwa kama njia ya ukombozi kwa wananchi wa Makurumla,” anasema.

Usalama wa watoto na elimu

Katika kukabiliana na taharuki ya utekaji watoto, Kimwanga anasema alifanya mikutano na wazazi, walezi na walimu katika shule za msingi za Mianzini, Karume na Dkt. Omari.

Anasema katika mikutano hiyo, alitoa wito kwa jamii kuhakikisha usalama wa watoto na kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama.

Kituo cha Afya Mburahati

Kimwanga anasema ameunga mkono juhudi za kuboresha Kituo cha Afya cha Makurumla, ambacho kilipandishwa hadhi kutoka zahanati hadi kituo cha afya mwaka 2016.

“Kituo hiki kinahudumia watu kati ya 250 hadi 300 kwa siku na sasa tayari kupitia halmashauri wakati wowote tutapokea gari jipya la wagonjwa pamoja na jenereta la dharura la thamani ya zaidi ya shilingi milioni 100 na sehemu

ya uchunguzi wa magonjwa kama vile x-ray, ultrasound, maabara,” anasema.

Kwa upande wa CCM, Kimwanga anasema ameweza kutoa kompyuta kwa matawi yote 10 ya CCM kama njia ya kukifanya chama kuwa cha kisasa zaidi hasa kwenye zama hizi za teknolojia.

Michezo na burudani


Kupitia “Kimwanga Cup” ambayo alianzisha mwenyewe na kupitia mashindano ya mpira wa miguu yaliyofanyika katika misimu tofauti, lengo likiwa ni kuibua vipaji na kuimarisha mshikamano wa vijana, wamefanikiwa kutoa ng’ombe mwenye thamani ya shilingi milioni moja.

Katika mashindano haya, anasema timu ya Mingle FC iliibuka mshindi na kupewa zawadi ya ng’ombe, jambo lililovutia hisia za mashabiki wengi wa soka.

Ushirikiano na Serikali Kuu

Kimwanga anaishukuru serikali ya awamu ya sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuendelea kutoa fedha za maendeleo katika Kata ya Makurumla.

“Napongeza hatua mbalimbali zinazochukuliwa na viongozi wa kata katika kusimamia miradi ya maendeleo, ikiwemo miundombinu mbalimbali, kipekee Mbunge wa Ubungo, Profesa Kitila Mkumbo, ambaye amekuwa kiungo muhimu katika gurudumu la maendeleo kwa wananchi wa kata zote za Jimbo la Ubungo,” anasema Kimwanga.

Habari**Joto la uchaguzi CCM sasa lapanda****Dkt. Angeline Mabula****Paul Makonda****Lazaro Nyalandu****Daniel Chongolo****Jesca Magufuli****Doto Biteko****Na Mwandishi WETU**

JOTO la Uchaguzi Mkuu limeanza kupanda baada ya pazia la kuchukua fomu za kuwania ubunge, udiwani kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) kufunguliwa rasmi Juni 28, 2025.

Mawaziri wa zamani, wafanyabiashara na waliowahi kuwa watumishi wa umma, wameonekana kupishana kwenye milango ya ofisi za chama hicho tawala kuchukua fomu za kuwania dhamana za kuongoza wananchi katika maeneo mbalimbali.

Miongoni mwa wanasiasa wakongwe na waliopata kuwa wabunge na kushika nafasi ya

uwaziri ni pamoja na aliyewahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Lazaro Nyalandu.

Nyalandu aliyewahi kuwa Mbunge wa Singida Kaskazini (sasa Ilongero) kwa vipindi viwili na baadaye kugombea urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, amechukua fomu ya kuwania ubunge katika jimbo hilo la Ilongero.

Nyalandu alikabidhiwa fomu hiyo juzi na Katibu wa CCM Wilaya, Hanzurun Mtebwa.

Waziri mwingine wa zamani aliyechukua fomu ya kuwania ubunge ambaye naye aliwahi kuwa Waziri wa Maliasili na Utalii, Ezekiel Maige.

Maige ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Msalala, Shinyanga kuanzia mwaka 2005-2020, amechukua fomu tena ya kuomba ridhaa ya kuwania ubunge wa jimbo hilo.

Alikabidhiwa fomu hiyo juzi na Katibu wa CCM Wilaya ya Kahama, Andrew Chatwanga.

Aliyekuwa Waziri wa Mambo ya Ndani na Mbunge wa Mwibara kwa vipindi viwili kuanzia 2010-2020, Kangi Lugola naye ni miongoni mwa waliochukua fomu akiwania tena jimbo hilo la Mwibara, Mara.

Mwingine aliyechukua fomu katika jimbo hilo ni pamoja na Cyprian Musiba.

Dkt. Angeline Mabula aliyewahi kuwa Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na baadaye kuwa waziri kamili, naye amechukua fomu ya kuwania uteuzi wa nafasi ya ubunge katika Jimbo la Ilemela mkoani Mwanza akitetea nafasi yake.

Mjumbe wa Halmashauri Kuu ya CCM (NEC), Leonard Qwihaya maarufu Manguzo, naye amechukua fomu kuwania jimbo hilo la Ilemela.

Aliyekuwa Mbunge wa Shinyanga Mjini kwa vipindi viwili kuanzia 2010-2020 na Makamu wa Rais wa Bunge la Afrika (PAP), Stephen Masele naye amechukua fomu ya kuwania tena ubunge katika jimbo hilo Shinyanga Mjini.

Spika wa Bunge la 12, Dkt. Tulia Ackson naye amechukua fomu ya kuomba kuteuliwa kugombea ubunge katika jimbo jipya la Uyole.

Joto la uchaguzi

Inatoka Uk. 24

Mwingine ni aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalumu kupitia Chadema, Ester Bulaya ambaye amerudi CCM na kuchukua fomu ya kugombea ubunge Jimbo la Bunda Mjini, Mara.

Bulaya aliyepata kuwa mbunge wa viti maalum (CCM) mwaka 2010 hadi 2015, kabla ya mwaka 2015 kuhamia Chadema na baadaye kugombea ubunge wa Bunda Mjini huku akimshinda mwanasiasa mkongwe, Stephen Wasira, ambaye sasa ni Makamu Mwenyekiti wa CCM.

Baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kumalizika, Bulaya na wenzake 18 waliingia katika mgogoro na Chadema baada ya kuapishwa kuwa wabunge wa viti maalum pasipo kuruhusiwa na chama hicho kikuu cha upinzani.

Aliyewahi kuwa Mbunge wa Iringa Mjini kupitia Chadema, Mchungaji Peter Msigwa ambaye kwa sasa ni kada wa CCM, naye amechukua fomu ya kuwania ubunge katika jimbo hilo kupitia chama hicho tawala.

Wengine waliochukua fomu za ubunge ni pamoja na Miriam Mjema, Jimbo la Same Mashariki na Anna Kilango Malecela ambaye anatetea nafasi yake.

Waliochukua fomu Same Magharibi ni pamoja na Yusto Mapande na Profesa Ladslaus Mnyone, huku Dkt. David Mathayo naye akitetea nafasi yake.

Waliojitokeza kuchukua fomu Jimbo la Vunjo ni pamoja na Yuvenal Shirima, Diddas Lyamuya, Obrey Silayo na Lucy Mrema, huku Jimbo la Moshi Vijijini wakichukua Enock Koola, Deogratius Mushi, Abdon Mallya, Nicodemus Masao na Gloria Mushi.

Miongoni mwa waliojitokeza kuchukua fomu za kuwania ubunge wa viti maalum ni Jesca Magufuli ambaye ni mtoto wa Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Magufuli.

Jesca amechukua fomu juzi akiomba kuteuliwa kugombea ubunge wa viti maalum kupitia Umoja wa Vijana CCM (UVCCM) Taifa.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo amechukua fomu ya uteuzi kwa ajili ya kugombea ubunge Jimbo la Makambako, Njombe. Chongolo ambaye amewahi kuwa Katibu Mkuu



Ester Bulaya



Masanja Kadogosa

wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), amekabidhiwa fomu hiyo juzi na Katibu wa CCM Wilaya ya Njombe, Mariam Kireti.

Kulwa Biteko pacha wa Naibu Waziri Mkuu, Dotto Biteko, naye amechukua fomu jimbo jipya la Katoro. Kulwa, ambaye mwaka 2020 alijitosa kuwania nafasi hiyo, fomu na Katibu wa CCM Wilaya, Michael Msuya.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa naye amejitosa kuwania ubunge Jimbo la Bariadi Vijijini. Kadogosa alikabidhiwa fomu hiyo juzi Juni 28, 2025 na Katibu wa CCM, Wilaya ya Bariadi, Ibrahim Kijanga.

Furaha Domnick, mpwa wa Rais wa Awamu ya Tano, Dkt. John Magufuli, amechukua fomu ya kuwania ubunge katika Jimbo la Kawe, Dar es Salaam.

Mwingine aliyechukua fomu akiomba kuwania ubunge katika jimbo hilo ni Gaston Francis.

Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Paul Makonda amechukua fomu ya uteuzi kwa ajili ya kugombea ubunge katika Jimbo la Arusha Mjini. Makonda, ambaye amewahi kuwa Katibu wa NEC ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, alikabidhiwa fomu hiyo juzi na Katibu wa CCM Wilaya ya Arusha Mjini, Timothy Sanga.

Wakati watia nia hao wakiendelea kuchukua fomu, Katibu wa NEC ya CCM, Itikadi, Uenezi na Mafunzo, Amos Makalla, amewaonya wataendaji wanaowatoza wanachama fedha zaidi ya kiwango kilichowekwa cha ada ya fomu.

Imeelezwa kuwa baadhi ya wagombea wanaokwenda kwenye ofisi za CCM kwa ajili ya kuchukua fomu wamekuwa wakitozwa zaidi ya viwango vilivyowekwa na chama hicho.

Viwango vya fomu vilivyopangwa ni shilingi 500,000 kwa nafasi ya ubunge na shilingi 50,000 kwa madiwani, lakini tayari yamesikika malalamiko ya baadhi ya wagombea kutozwa zaidi.

Habari katika picha

Baadhi ya wanafunzi na abiria waliokuwa kwenye gari la Shule ya Chalinze Modern Islamic Primary School, wakipatiwa huduma ya kwanza baada ya gari lao kupata ajali eneo la Kimara Suka jijini Dar es Salaam juzi. (Picha na Fidelis FELIX)



Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Christina Musyani kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dodoma akizungumza na maafisa, wakaguzi na askari jinsi ya kutoa huduma bora kwa jamii wakati wa kikao kazi kilichofanyika Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe, mwishoni mwa wiki. Na Mpigapicha Wetu



Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi (SACP), Christina Musyani kutoka Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dodoma akizungumza na maafisa, wakaguzi na askari jinsi ya kutoa huduma bora kwa jamii wakati wa kikao kazi kilichofanyika Wilaya ya Mbozi, mkoani Songwe, mwishoni mwa wiki. Na Mpigapicha Wetu



Mwenyekiti wa Chadema, Tundu Lissu, akitoka nje ya Mahakama Kuu baada ya kusikiliza mapitio ya mwenendo wa kesi ya uchochezi namba 8606/2025, Dar es Salaam Ijumaa iliyopita. (Picha na Fidelis Felix)



Viongozi wakimsikiliza Rais Samia Suluhu Hassan wakati akihitimisha shughuli za Bunge la 12 la Jijini Dodoma mwishoni mwa wiki. Picha na Ikulu

Na Rashid
MTAGALUKA

Hoja Yangu

Wasiowajibika kikwazo kwa maendeleo



Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Charles Kichere

KATIKA nchi yoyote inayolenga maendeleo ya kweli, uwajibikaji wa watendaji wa serikali ni msingi imara wa mafanikio.

Hata hivyo, Tanzania bado inakumbwa na tatizo sugu la baadhi ya watendaji wanaofanya kazi kwa mazoea, kusubiri ziara za viongozi wakuu wa kitaifa au wa mkoa ili waonyeshe kile kinachoonekana kama 'uwajibikaji wa ghafla'.

Hakika tabia hii siyo tu ya kusikitisha, bali pia ni dalili ya uzembe, usaliti kwa kiapo cha uongozi, na kikwazo kikubwa kwa maendeleo ya wananchi.

Mfano wa hivi karibuni unaoibua maswali mengi kuhusu utendaji wa serikali ni ule wa Maadhimisho ya Miaka 20 ya Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (MUM) yaliyofanyika Ijumaa ya Juni 20, 2025.

Kipande kifupi cha barabara ya takriban mita 500 kutoka stendi ya Dodoma kuelekea MUM kupitia kituo cha Tanesco kilikuwa katika hali mbaya kwa muda mrefu, kikiwa na mahandaki ya kutishia usalama wa magari na watu.

Licha ya eneo hili kuwa la kimkakati, likihudumia wanafunzi, watumishi wa chuo, na wakazi wa maeneo jirani, hakuna hatua zilizo-chukuliwa, hadi pale ilipofahamika kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa atakuwepo akiwa mgeni rasmi katika sherehe hizo.

Ghafla, shughuli za kufukia makorongo zikaanza kana kwamba ukarabati wa miundombinu ni jambo la dharura tu wakati wa ujio wa viongozi wakuu.

Tabia hii ya 'kujipamba kwa ajili ya mgeni' ni kama sarakasi za kisiasa zisizo na tija kwa mwana-nchi wa kawaida.

Kwa mujibu wa takwimu za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) za mwaka 2023/2024, zaidi ya asilimia 30 ya miradi ya barabara inayoangukia chini ya Tarura haikukamilika kwa wakati, huku sababu kubwa zikitajwa kuwa ni usimamizi mbovu na ukosefu wa uzalendo miongoni mwa baadhi ya watendaji.

Kwa nini barabara au majengo ya shule, zahanati na taasisi nyingine zisafishwe au kufanyiwa ukarabati kwa sababu tu kuna ujio wa Mwenge wa Uhuru au viongozi wa kitaifa?

Mbona wananchi wapo hapo kila siku? Hii ni kudhihirisha kuwa baadhi ya watendaji wamejisahau, hawajali maslahi ya umma, na wamegeuza utumishi wa umma kuwa nafasi ya kujitafutia maslahi binafsi badala ya kuhudumia wananchi.

Tatizo hili limekithiri hadi kuwakatisha tamaa wananchi. Wengine wanauliza kwa kejeli: "Je, tunahitaji waziri mkuu aje kila wiki ili barabara zitengenezwe au shule zipakwe rangi?" Kauli kama hizi zinaashiria kukosekana kwa imani ya wananchi kwa baadhi ya viongozi wa mikoa, wilaya na halmashauri.

Ni wakati sasa mamlaka zinazohusika kama Ofisi ya Rais – Tamisemi, na hata Ofisi ya Waziri Mkuu, zikaweka utaratibu wa wazi wa kuwabaini na kuwaondoa watendaji wa namna hii.

Taifa letu halihitaji viongozi wa maonyesho, bali wale wanaofanya kazi.

Mwandishi anapatikana kwa simu nambari 0784 438 546 na email; mtagaluka@gmail.com

Riwaya

Viaticum-40

Sakramenti ya Mwisho



KWA wasomaji wapya: Polisi wanaendelea na kazi zao na huku Eddy akiendelea na majukumu yake kukusanya taarifa kwa ajili ya gazeti lao la Mizani. Je, nini kitaendelea? Ungana na mtunzi kufaidi riwaya hii kali ya uchunguzi.

Na Godwin Chilewa, Houston, MAREKANI

KABLA ya kwenda kulala, Eddy aliamua kufanya mambo mawili muhimu; kwanza alimpigia simu Stella kumueleza mambo yaliyokuwa yakiendelea.

Haja yake hasa ilikuwa kumtaka aweke kumbukumbu za mambo yote ili baadaye waweze kuchuja na yale ya muhimu yatumike katika habari au makala zitakazoandikwa baadaye. Utaratibu huu uliwasaidia pia kwa mambo ya kiusalama.

Baada ya kuzungumza na Stella, akapiga simu Kituo Kikuu cha Polisi Mwanza, kuulizia taarifa za kifo cha Dokta Evance Mushi.

Hapa lengo kubwa ilikuwa kupata taarifa za jinsi ajali hiyo ilivyotokea, na kama dereva aliyeshababisha ajali hiyo alishapatikana.

Kwa bahati mbaya, askari aliyepokea simu alikuwa mkorofi sana. Pamoja na Eddy kujitambuliisha kwamba ni mwandishi wa Habari, polisi huyo hakutaka kumsikiliza, wala kumpa taarifa yoyote.

Alimtukana tu, halafu akakata simu.

Kitendo hicho kilimsikitisha sana. Hakuna kitu kilichokuwa kikimkera kama kushughulika na watumishi wa serikali wanaosahau kwamba nao ni sehemu ya jamii, na kuwa mamlaka waliyonayo yanatoka kwa wananchi.

“Laiti kama askari huyo angejua Mizani limechangia kwa kiasi gani kuboreshwa kwa mishahara yao na watumishi wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama, bila shaka asingenibeza hivi,” alifikiri.

Eddy akakumbuka jinsi makala za Inspekta Hatibu zilivyowasumbua wabunge, na viongozi wengine wa kitaifa mpaka wakakubali kupandisha mishahara ya watumishi kwa asilimia sitini.

Jambo lililokuwa halijawahi kutokea katika historia.

Wakati akiendelea kumfikiria askari huyo, akakumbuka watoa habari walionao katika ofisi za serikali, mashirika ya umma, na vyombo mbalimbali vya ulinzi na usalama, ikiwa pamoja na Jeshi la Polisi.

Watoa habari hawa kwa ujumla ndiyo ilikuwa chachu ya mafanikio yea mafanikio ya Mizani. Ushirikiano wao uliwezesha kupatikanakwa taarifa za ndani ya serikali, taasisi za umma na hata ikulu.

Kimsingi investigative journalism haina tofauti na ukachero au ujasusi. Ili kupata habari za maana, ni lazima chombo kiwe na vyanzo vya uhakika katika kila sehemu nyeti.

Hilo ndilo lililofanya Mizani iajiri waandishi wa habari mahiri na wenye uhakika nchi nzima.

Miaka miwili iliyopita, Mizani ilikuwa na watoa habari wa maana sana mkoani mwanza. Mmojawapo alikuwa ofisa wa Polisi mwenye cheo cha Mrakibu wa Polisi Kwa bahati nzuri ofisa huyo alipandishwa cheo kuwa Mrakibu Mwandamizi wa Polisi (SSP), akahamishiwa Tarime, alikopewa ukamanda wa wilaya.

Bahati nzuri kabla ya kuondoka Mwanza, ofisa huyo alimtambulisha Eddy kwa askari wengine wawili aliokuwa akiwaamini sana; wa kwanza alikuwa mkaguzi wa polisi aitwae Robert mwenye umri wa miaka arobaini, na wa pili alikuwa sajeni, kijana mwenye umri wa miaka ishirini na tano maarufu kwa jina la Machafuko.

Inaendelea Uk. 29

Viaticum-40

Sakramenti ya Mwisho

Inatoka Uk. 28

Basi, Mizani iliwafanyia upekuzi wa kina, ilipojiridhisha ikawaingiza kwenye mtandao na kuanza kuwatumia.

Kwa vile Eddy hakuwa mkazi wa Mwanza, aliwakabidhi watoa habari hao kwa mwakilishi wao ili aweze kuwatumia.

Hata hivyo, kila ilipowezekana, Eddy mwenyewe aliwatafuta akazungumza nao kuwa pa malengo, na mara myingine aliwaalika Dar es Salaam kuwapa ukarimu wa kiwango cha juu bila kuwaumbua.

Kwa mambo yaliyotokea usiku huu, Eddy aliona vyema kumpigia simu Machafuko, maa-na alikuwa kijana zaidi, damu ilikuwa ikichemka mwilini mwake.

Pamoja na hilo, hakuwa na mke wa kumbana au kumuuliza maswali mengi. Alikuwa huru kufanya mambo mengi kuliko Inspekta Robert.

Basi, akatoa simu yake ya mkononi, lakini kabla hajabonyeza namba za machafuko wazo lingine likamjia.

Akarudisha simu yake mfukoni, akatembea kuelekea mapokezi, akatumia simu ya hapo kumpigia Machafuko.

“Halow, habari yako,” Machafuko aliongea mara tu baada ya kuweka iPod yake sikioni.

“Salama kabisa, ila haya mambo ya kuchanganya konyagi na soda siyo mazuri hata kidogo,” Eddy alimjibu kwa sauti ya utulivu.

“Nilifikiri umeacha pombe kali?” Machafuko aliuliza.

“Bia zimepanda bei mno, nimeona bora nianze kunywa konyagi”

“Mimi nimeacha kunywa hata CocaCola.”

“Bila shaka umekuwa Msabato, au mlokole.”

“Ni kweli, familia haijambo? Machafuko aliuliza kwa sauti ya upole kama mtu anayeongea na mzazi wake.

“Nina salamu kutoka kwa mchumba wako.”

“Uko mjini hapa?”

“Nimeshakuwa mwenyeji, tunaweza kuonana?”

“Usiku huu? Aliuliza kwa mshangao.

“Ndiyo, mwenzio mjamzito, na bado hamjafunga ndoa, amechanganyikiwa vibaya mno.”

“Ndiyo kwanza natoka kazini, lakini tunaweza kuonana baada ya nusu saa, kama ni lazima tuonane leo.”

“Ni muhimu, tafadhali tuonane japo kwa dakika tano.”

“Nitakuwa kwa mama ntilie baada ya nusu saa.”

“Ahsante, tukutane hapo,” Eddy akakata simu.

Pamoja na umri wake mdogo, askari huyu alikuwa akimvutia sana. Bidii na uhodari wake katika kazi, ni jambo lililokuwa halifichiki.

Zaidi ya yote alikuwa na uwezo mkubwa wa kufikiri haraka, kupambanua mambo na kufanya maamuzi sahihi.

Ukichanganya na shahada yake ya sheria kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kijana huyu alikuwa na nafasi nzuri ya kupanda cheo na kuwa mtu mkubwa katika jeshi hapo baadaye.

Kwa mama ntilie walikokubaliana kukutana hapakuwa mbali na hoteli aliyofikia, yapata mwendo wa dakika tano tu kwa gari au pikipiki.

Kwa hiyo, Eddy hakufanya haraka kuondoka. Akasubiri hotelini hapo mpaka zilipobaki dakika kumi ndipo akatoka nje, akaita taksi, akamwambia dereva ampeleke ferry.

Walipofika, akamlipa ujira wake, akateremka, akaingia mtaani.

Kwa kawaida eneo hili huwa na pilika nyingi wakati wote. Mamia ya wafanyabiashara ndogondogo, maarufu kwa jina la wamachinga, wachuuza samaki, kina mama ntilie, na hata machangu-doa walikuwa kwenye pilikapilika za kujipatia fedha kutoka kwa wasafiri wanaosubiri ferry, na wenyeji waliochelewa kurudi majumbani mwao kwa sababu mbalimbali.

Kila Eddy alipopiga hatua chache mmojawapo wa wachuuzi alimsimamisha kumshawishi anunue bidhaa anazouza. Alimkuta Machafuko ameshafika mahali walipokubaliana. Alipomkaribia kijana huyo akageuka, akaanza kutembea taratibu kuelekea upande wa pili.

Eddy akamfuata taratibu mpaka wakatoka kabisa katika eneo hilo. Hapo Eddy akaongeza mwendo mpaka akamkuta.

Itaendelea...

Kuelekea Uchaguzi 2025**Mwandishi kuwavaa vigogo Mwibara**

*Mwanahabari,
Maregesi Paul*

Na Rachel MRISHO

KIPYENGA cha kuomba ridhaa ya wanachama wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuomba ridhaa kuteuliwa kukiwakilisha, kimepulizwa.

Watia ni wengi na mmoja wao ni mwandishi wa habari mwandamizi, Maregesi Paul, ambaye anawania ubunge katika Jimbo la Mwibara, lili-lopo wilayani Bunda, Mara.

Pambazuko limemhojiano mtia nia huyo, ambaye mbali na mambo mengine, ameeleza mipango na mikakati aliyonayo ya kuleta mabadiliko na maendeleo katika jimbo hilo. Fuatilia mahojiano haya;

Pambazuko: Wewe ni mwandishi wa habari mwandamizi, nini kimekusukuma kuwania ubunge?

Maregesi: Kwanza ni haki yangu ya kikatiba kuwania nafasi hiyo na pia nchi yetu inaruhusu mwana CCM kutumia haki yake ya kikatiba kugombea na kuchaguliwa katika nyanja mbalimbali za uongozi ndani ya chama.

Kwa kuwa mimi ni raia halali wa Tanzania, naitumia haki hiyo kuwania ubunge katika Jimbo la Mwibara.

Pambazuko: Majukumu ya ubunge na uandishi wa habari msingi wake mkuu ni kuwazungumzia wananchi. Ni kwa nini umefikiria kuwania ubunge badala ya kuendelea na uandishi wa

habari?

Maregesi: Wajibu wa mwandishi wa habari ni kuhabarisha umma, kuibua kero na changamoto mbalimbali zinazowakabili wananchi na kuzifikisha kwa watoa maamuzi na kuhakikisha zinatatuliwa.

Ubunge ni daraja kati ya Serikali na wananchi, hivyo wajibu wa mbunge ni kuwakilisha wananchi bungeni, yaani kuwasemea wananchi moja kwa moja serikalini kuhusu kero na changamoto zinazowakabili majimboni.

Kutokana na mazingira yaliyoko Mwibara ambako ndiko asili yangu, nimekaa na kutafakari kwa kina na kuamua kwamba, ni wakati mwafaka kwangu kuwania nafasi ya ubunge ili nikawawakilishe wananchi wa Mwibara, katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Msukumo wangu umetokana na hali ninayotia jimboni kwetu ambako kuna changamoto nyingi ambazo hazijashughulikiwa kwa miaka mingi.

Kwa hiyo, kupitia kazi yangu ya uandishi wa habari, nimekuwa nikifuatilia na kuripoti habari za Bunge huku nikiwasikiliza wabunge wa Mwibara waliopita na kuona namna wanavyowawakilisha wananchi wa Mwibara.

Kwa bahati mbaya, sijaona ushawishi wao kwa serikali, hivyo nimejiridhisha pasi na shaka na kuona kuwa inahitajika nguvu ya kijana mwenye utashi na ushawishi mkubwa na si mwingine bali ni mimi mwana-Mwibara, Maregesi Paul, ambaye wengi wananjua kama Mtoto wa Mvuvi.

Kwa kutumia taaluma yangu ya uandishi wa habari, naamini nitakuwa chachu ya kuishawishi serikali kushughulikia kero zinazolikabili Jimbo la Mwibara na viunga vyake.

Pambazuko: Ni changamoto gani zinazolikabili jimbo la Mwibara. Je, mikakati yako ni ipi katika kuzitatua?

Maregesi: Miongoni mwa mambo yaliyoni shawishi niwanie ubunge hasa ni kutokana na jamii ya Mwibara kuwa na malalamiko ya miaka mingi katika nyanja ya kilimo, elimu, afya, miundombinu na uvuvi.

Inaendelea Uk. 31

Kuelekea Uchaguzi 2025

Mwandishi kuwavaa...

Inatoka Uk. 30

Kwa mfano, katika jimbo la Mwibara vijiji vingi viko kandokando ya Ziwa Victoria, vijiji hivyo ni pamoja na Buzimbwe, Bulamba, Mwiseni, Kasuguti, Mahyoro, Namitwebili, Kasahunga, Kibara, Busambara, Bunere, Nambaza, Nansimo, Genge, Mwitende, Makwa, Kabilizi, Masahunga, Sunsi, Nambubi, Nampangara, Mchigondo, Bulegea, Sikiro, Mgara, Isanju, Nyalugoma, Mwiluluma, Mlanda na vingine vingi.

Pamoja na vijiji hivyo kuwa kandokando ya ziwa, kwa bahati mbaya sana havina maji ya uhakika ambayo ni safi na salama, badala yake wananchi wamekuwa wakitumia maji hayo ambayo yanaathiri afya zao.

Hebu jiulize, vijiji hivyo vinakosaje maji ilhali kuna chanzo cha maji cha uhakika kutoka katika ziwa hilo?

Inashangaza sana kuona maji yanayotoka Ziwa Victoria yasafirishwa kupelekwa mikoa ya Shinyanga na Tabora na kuwaacha wananchi wa Mwibara wakikosa huduma hiyo muhimu.

Mungu akinisaidia jina langu likipita na wananchi wakaridhia niwe mbunge wao, nitasimamia na kuhakikisha huduma hiyo inawafikia wananchi ambao ndio wanapaswa kuwa wanufaika wakuu.

Yawezekana jamii wasiamini au wakadhani kuwa jambo hili ni gumu na haliwezekani, lakini, kwa kuwa mimi ni mwanahabari, naami ni moja ya mambo mepesi kutekeleza ni hili la kuwafikishia wananchi huduma ya maji kutoka kwenye chanzo cha ziwa letu.

Pambazuko: Wananchi wa Mwibara wanategemea nini kukuza uchumi wao? Je, umejipangaje kuwawezesha ili kuchochea ukuaji zaidi wa uchumi?

Maregesi: Ziwa Victoria ni moja ya vitega uchumi katika jimbo la Mwibara, uchumi wa wananchi mbali na mambo mengine unategemea uvuvi.

Ziwa Victoria lina Samaki wa aina mbalimbali kama sangara, sato, dagaa, kamongo na wengine ambao husafirishwa nje ya nchi.

Lakini, kutokana na hali duni ya wananchi wa Mwibara, uvuvi wanaoufanya ni wa kienye-

ji zaidi kwani wanatumia zana hafifu na za kizamani ambazo zinawafanya wasinufaike na uvuvi huo.

Natamani sana wananchi waondokane na uvuvi huo na nikifanikiwa kuwa mbunge, nitawasaidia wavuvi kuvua kisasa ikiwa ni pamoja na kutumia vizimba ambavyo ndiyo kipaumbele cha Serikali kwa sasa.

Uvuvi wa vizimba unalipa, ila tatizo jamii haijapata elimu kuhusu uvuvi huu ambao una tija zaidi.

Vile vile, kupitia wataalamu wa uvuvi ninafahamiana nao, nitawasaidia wananchi kupata elimu ya kisasa ya uvuvi wa mabwawa kwani kwa bahati nzuri wanaonifahamu pale nyumbani kwetu katika Kijiji cha Nansimo tuna mabwawa ya Samaki.

Hivyo ninaposema nitawasaidia wananchi katika sekta hiyo, namaanisha kwani nina uzoe-fu mkubwa juu ya jambo hili.

Pamoja na hayo, mimi nimetoka kwenye familia ya wavuvi, nafahamu faida na umuhimu wa uvuvi katika kukuza uchumi wa familia na kipato cha mtu mmoja mmoja ndiyo maana nimeathamiria kuleta mabadiliko katika sekta ya uvuvi.

Kupitia sekta hiyo ya uvuvi, nitajitahidi kuwawezesha na kuwasaidia wavuvi kuunda vikundi ili Serikali ivitambue na kuviwezesha kiuchumi.

Ukiacha biashara inayotokana na uvuvi wa samaki, wananchi wa Mwibara wanategemea zao kuu la biashara la pamba.

Tatizo la zao hilo lipo katika bei kwani mara nyingi bei huwa hazitabiriki, yaani wakati mwingine zinapanda na kushuka.

Zao hilo naliunga mkono kwa sababu linachangia pato la Taifa, lakini kuna haja ya kutafuta zao jingine la biashara litakalochochea ukuaji wa uchumi ili mzunguko wa fedha ukue zaidi.

Hili nalo linawezekana kwa kuwatumia wataalamu wa kilimo ambao nimekuwa nao karibu sana katika shughuli zangu za uandishi wa habari.

Pambazuko: Hali ya miundombinu ya barabara na vivuko ikoje?

Inaendelea Uk. 32

Kuelekea Uchaguzi 2025

Mwandishi kuwavaa...

Inatoka Uk. 31

Maregesi: Miundombinu mizuri na wezeshi hasa ya barabara ni miongoni mwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi katika maeneo mbalimbali.

Mwibara kuna barabara moja tu inayoamini-ka ambayo ni inayotoka Bunda kuelekea Kisorya Kivukoni.

Lakini, barabara zinazounganisha vijiji kwa vijiji zina changamoto ambazo zinahitaji kutatuliwa.

Kwa mfano, barabara inayotokea kijiji cha Bulamba kupitia Kabainja kuelekea Ragata hadi Karukekere hadi Mwiruruma, ina changamoto zinazohitaji kutatuliwa.

Barabara nyingine ni ile inayotoka Kijiji cha Busambara kuelekea Kata ya Iramba ambayo nayo inahitaji matengenezo ili iweze kutumika majira yote ya mwaka.

Kuna barabara nyingine inayotoka Kijiji cha Nakatuba kuelekea Igundu hadi Namarama, nayo ina changamoto ya mashimo.

Kwa kifupi ni kwamba, barabara nilizotaja ni chache, lakini hili suala la ubovu wa miundombinu ya barabara, kwa kweli ni kero kwa wananchi wetu na ndoto yangu natamani ifike wakati lifanyiwe kazi na ibaki kuwa historia, hakuna wa kufanya hayo bali naona mimi nitamudu kazi hiyo.

Kwa upande wa vivuko mwibara kuna visiwa kama Nafuba, Nyamuguma, Buyanza, Sozisha na vingine ambavyo ili ufike huko, unahitaji kupanda boti.

Siyo kwamba boti hazipo, zipo bali zinahitajika zaidi hivyo nitakaa na wadau wa vyombo hivyo ili tuweze kuona namna nzuri ya kuboresha huduma hiyo kwa wananchi.

Pambazuko: Suala la afya kwa jamii limebeba

nafasi kubwa kwenye maisha ya wananchi. Nini mikakati na mipango yako katika jambo hilo?

Maregesi: Sekta ya afya ina changamoto ya uhaba wa wauguzi, waganga, ukosefu wa dawa pamoja na uhaba wa nyumba za watumishi hao.

Kama nilivyoeleza awali, kero ya maji inazikumba hospitali, zahanati na vituo vya afya katika jimbo letu.

Taaluma yangu ya uandishi wa habari ime-nikutanisha na watu wa kada nyingi, kwa hiyo, nitatumia nafasi hiyo kuishawishi Serikali itatue matatizo hayo kadiri itakavyowezezana.

Pambazuko: Vipi hali ya elimu jimboni humo, changamoto kubwa ni zipi na utazitatuaje?

Maregesi: Kwanza kabisa, dhamira yangu kubwa ni kuhakikisha wananchi wa Mwibara wanapata elimu bora, leo hii mimi nimetangaza nia ya kugombea ubunge nikiwa najiamini kutokana na elimu niliyonayo.

Siwezi kuwa mbinafsi wa kufurahia matunda ya elimu yangu bila kuweka ushawishi kwa wananchi wetu kuthamini elimu.

Licha ya kuwa sekta ya elimu ina uhaba wa walimu, ukosefu wa madawati, miundombinu ya madarasa kutokuwa mizuri, wazazi kutokuwa na mwamko wa kuchangia maendeleo ya elimu, naamini haya yote yanahitaji mtu sahihi wa kuyasemea na kuyafanyia kazi ambaye ni mimi mwenyewe.

Naendelea kusema na kusesitiza kuwa, mtu sahihi ni mimi, najivunia mtandao mpana nilionao kupitia taaluma yangu ya uandishi wa Habari.


Nitaishawishi serikali na wadau mbalimbali wa elimu ili kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto hizo.

Uhaba wa walimu nitaanza kwa kuwatumia vijana waliohitimu vyo vikuu na wenye elimu ya kati kufundisha kwenye shule zenye changamoto kubwa ya walimu hususani wenye uwezo katika masomo ya sayansi na hesabu.

Inaendelea Uk. 35



Habarika kidijitali! Soma gazeti la **Pambazuko** na magazeti mengine maarufu kwenye **Rifaly!**



Scan to download Rifaly

www.rifaly.com



Mambo muhimu Bunge la 12



Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Ackson

Na Mwandishi WETU

RAIS Samia Suluhu Hassan amehitimisha uko-mo wa Bunge la 12 la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania – Ijumaa iliyopita, Juni 27.

Katika hotuba yake ndani ya Bunge, Rais Samia alitumia muda mrefu kuonesha mafanikio ya serikali kwa kipindi cha karibu miaka minne na nusu akiwa kiongozi wa Tanzania.

Wakati akihitimisha, Rais Samia alieleza yale aliyoyasimamia katika kipindi chake, lakini bila kukwepa kipindi cha mtangulizi wake, Rais John Magufuli aliyanzisha safari ya miaka mitano ya Bunge la 11 na baadaye muda mfupi wa Bunge la 12 lililoanza 2020.

Takribani saa 2.50, Rais Samia alizotumia kueleza utekelezaji wa Ilani ya CCM kwa bunge hilo - akiwa amesimama kwa muda wote, alieleza kwa mapana na marefu safari ya miaka 10 ya serikali, chini ya bunge hili, hasa kwa kuangazia mafanikio yaliyofikiwa katika kipindi hicho, ambayo kwa lugha nyepesi yeyote anaweza kusema “siyo mafanikio haba.”

Safari hii inajumuisha kazi iliyifanywa na mabunge mawili; Bunge la 11 chini ya Magufuli, Rais Samia akiwa makamu wake, na Bunge la 12, ambalo Rais Samia alishika hatamu baada ya kifo cha Magufuli Machi 2021.

Rais Samia amevunja bunge hili, ambapo tofauti na mabunge yaliyotangulia, limeiacha alama ya kipekee katika historia ya Tanzania, ku-

tokana na mtiririko wa matukio yasiyotarajiwa, yaliyoibua historia mpya kwa taifa.

Bunge la 12 limeacha historia yake ya kipekee, likiwa na matukio ya kisiasa, kisheria na kijamii, ambayo yataendelea kukumbukwa kwa muda mrefu.

Bunge la marais wawili

Bunge hili la 12 linakuwa la namna yake likiwa limeshuhudia marais wawili, ambapo lilifunguliwa rasmi na Rais Magufuli Ijumaa Novemba 13, 2020 ikiwa ni muda mfupi baada ya kukamilika kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, likiwa chini ya Spika Job Ndugai.

Miezi mitano baadaye, kutokana na kifo cha Magufuli, Rais Samia ambaye alishika wadhifa huo alihutumia Bunge hilo Aprili 22, 2021 ikiwa ni muda mfupi baada ya kuapishwa kwake, Machi 19, 2021, wakati bunge hilo likiendelea kuwa chini ya Spika Ndugai.

Rais Samia alimalizia kwa kuhitimisha rasmi shughuli za bunge hilo Ijumaa Juni 27, 2025 kwa kutoa hotuba yake ya mwisho na kuwapa nafasi wabunge kurejea majimboni na kuendelea na hatua nyingine kuelekea Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu. Bunge la 12 lilianza rasmi shughuli zake Novemba 1, 2020.

Maspika wawili

Katika kipindi cha miaka mitano ya Bunge hili, limeshuhudia maspika wawili, akiwemo aliyekuwa Spika wa Sita, Job Ndugai ambaye ndiye mtangulizi wa Spika Tulia Ackson.

Ndugai ndiye aliyempokea Rais Samia alipo-hutubia Bunge kwa mara ya kwanza, lakini alilazimika kujiuzulu wadhifa huo Januari 6, 2022 kutokana na sababu za kisiasa.

Ndugai alijiuzulu nafasi hiyo siku chache baada ya kusambaa kwa video iliyomnukuu akisema kwamba “iko siku nchi itauzwa kutokana na madeni” baada ya serikali kwenda kukopa mikopo ya karibu trilioni 1.3 kwa ajili ya ujenzi wa madarasa na vituo vya afya, kauli ambayo ilijibiwa moja kwa moja na Rais Samia akieleza kushangaa kwake na kwamba asingetarajia kauli ya aina hiyo kutoka kwa Ndugai.

Habari**Mambo muhimu...****Inatoka Uk. 33**

Katika barua yake ya kujiuzulu, Ndugai alieleza kuwa alichukua uamuzi huo binafsi kwa hiyari, akizingatia maslahi mapana ya nchi, serikali na CCM.

Kutokana na hatua hiyo, Bunge lilimchagua aliyekuwa Naibu wa Spika, Dkt. Tulia Ackson kuwa Spika wa saba wa Bunge, ambaye alianzisha safari mpya, akilalamikiwa kwa kulifanya Bunge kuwa “mtetezi wa serikali” badala ya kuwa chombo cha kuiwajibisha Serikali.

Kukosa kambi rasmi ya upinzani

Kutokana na yale yaliyotokea katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2020, upande wa upinzani kwa Tanzania Bara ulipata kiti kimoja cha Aida Kenani (Nkasi Kaskazini-Chadema), hivyo kukosa uwezekano wa kuwa na kambi ya upinzani bungeni.

Kwa upande wa Zanzibar, walikuwepo wabunge saba ambao ni wa ACT –Wazalendo-wabunge wanne, na CUF kuwa na wabunge watatu, hivyo kufanya wabunge wa upinzania kufikia wanane.

Kati ya wabunge 264 wa kuchaguliwa, ni wanane tu waliotoka nje ya CCM, hivyo chama hicho kuwa na asilimia 97 ya wabunge wote.

Kwa hatua hiyo, Bunge hili lililazimika kutafuta wabunge watakaowakilisha upinzania na kuchukua wajumbe 19 kutoka Chadema ambao uteuzi wao ulilalamikiwa kwa kutofuata utaratibu baada ya chama chao kukana kupeleka majina yao bungeni, hivyo kusababisha kupewa jina la Covid-19.

Chadema ililazimika kuchukua hatua ikiwemo za kuwafikuza uanachama, lakini hatua hiyo haikutambuliwa na Spika baada ya wabunge hao kukimbilia mahakamani kupinga kufukuzwa kwao. Wabunge hao wameendelea kuwepo hadi bunge hili linapomaliza muda wake.

Inatambulika kwamba uwepo wa mbunge, wakiwemo wa viti maalumu, unabebwa na baraka za kisheria kutoka kwa chama na iwapo atafukuzwa uanachama wake, ubunge unakoma, ila kwa hawa 19 waliendelea kuhudhuria vikao vya Bunge la 12 hadi mwisho wa muhula wa bunge.

Mjadala iliyokosa nafasi

Katika Bunge hili la 12, baadhi ya mijadala iliyokuwa kilio cha umma haikupata nafasi. Mjadala hiyo ni pamoja na ile ya utekaji, watu kupotea na mauaji ya watu, hasa waliokuwa upande wa upinzani.

Bunge lililalamikiwa kupuuza matukio ya wazi ya utekaji, mateso na kupotea kwa wapinzani, wanaharakati na hata waandishi, huku baadhi ya wabunge wakisimama kidete kudai kuwa watu wanaotajwa kupotea walijiteka, kijipoteza au kujijeruhi.

Mjadala mwingine uliokuwa ukipigiwa kelele ni ule wa Mkataba wa DP World kutoka Dubai, kwa ajili ya usimamizi wa Bandari ya Dar es Salaam. Mkataba huu uliozua maswali mengi ya kisheria na kikatiba.

Mjadala mwingine uliokosa nafasi pamoja na kuwa na shinikizo kubwa la wananchi ni ule uliohusu malalamiko ya watu wa jamii za Kimsai waliokuwa wakidai kulazimishwa kuhama katika maeneo yao ya asili.

Wabunge waliojaribu kusimama kidete kutaka kushinikiza kuzungumzwa kwa hoja hizi bungeni, walijikuta matatani.

Wapo wanaoamini kuwa Bunge hili lilikosa eneo la kujikita na kukosa Kaulimbiu iliyoeleweka, kama ilivyokuwa kwa Bunge la tisa chini ya Spika Samuel Sitta (2005–2010) lililjulikana kwa kaulimbiu ya “Bunge la Kasi na Viwango” na hata lile la 10 na 11 lililoongozwa na spika wa kwanza mwanamke Tanzania, Anne Makinda.

Bunge la tisa la Spika Sitta, liliweza kuibua mijadala mizito kuhusu kashfa ya Richmond (2008) iliyomuondoa waziri mkuu wa wakati huo, Edward Lowassa na ile ya Escrow (2014), ambazo zilisababisha mawaziri na viongozi kadhaa wakuu kujiuzulu.

Lakini, Bunge la 12 lilionekana kukosa sauti mbadala kutokana na upungufu wa wabunge wa upinzani.

Mjadala mingi haikuwa na changamoto ya upande mwingine, jambo lililopunguza msimko na ufuatiliaji wa umma.

Na kwa sababu lilikuwa na wabunge wengi wa chama kimoja na wenye mtizamo mmoja kwa wengi wao, ilikuwa rahisi mijadala na hoja kupita kwa kishindo bila kupata upinzani wala mawazo mbadala.

Inaendelea Uk. 35

Mambo muhimu...



Inatoka Uk. 34

Mijadala tata

Licha ya changamoto, kukosa upinzani, laki-ni Bunge la 12 halikukosa mijadala na michango ya kuvutia ikiwemo michango yenye utata.

Mbunge wa Kinondoni, Abbas Tarimba alipendekeza wabunge wapate namba maalum za magari.

Mbunge wa Geita Vijijini, Joseph Musukuma aliomba wake wa wabunge watambuliwe kama watu mashuhuri (VIP) na wapewe hadhi hiyo wanapokuwa katika maeneo maalum, ikiwamo viwanja vya ndege.

Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Mjini Magharibi, Tauhida Gallos yeye alitumia neno “kenge” dhidi ya wanaharakati, akieleza namna anavyowachukia, kauli iliyozua mjadala mkali.

Tozo za miamala ya simu; mjadala huu uliwaweka wabunge kwenye ‘presha’ kubwa kutoka kwa wananchi, na serikali ililazimika kufanya marekebisho. Moja ya mijadala iliyopongezwa na wananchi.

Sakata la sukari; vuta nikuvute kati ya Mbunge Luaga Mpina na Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe kuhusu vibali vya sukari ilisababisha Mpina kusimamishwa bungeni.

Ripoti za CAG; hizi ziliibua hoja juu ya matumizi ya fedha za umma, lakini hazikufikia uzi-to wa miaka ya nyuma.

Sheria mpya za uchaguzi; Bunge hili pia lilipitisha sheria muhimu kama muswada wa Tume Huru ya Uchaguzi, sheria mpya ya uchaguzi wa rais, wabunge na madiwani, pamoja na marekebisho ya sheria ya vyama vya siasa.

Mwandishi kuwavaa...

Inatoka Uk. 32

Pambazuko: Unatarajia kufanya nini kutatua changamoto ya ukosefu wa ajira kwa vijana na kuwawezesha wanawake mitaji ya kibiashara?

Maregesi: Serikali haiwezi kuajiri kila mtu, kwa hiyo, nitatumia kila mbinu ikiwamo kutoa elimu ya namna ya kutumia fursa zilizopo jimboni kwetu kujiajiri na wakati huohuo nitawaunganisha kwenye vikundi vya kilimo, uvuvi na ufugaji. Kwa kupitia vikundi hivyo, wataalamu watawaelimisha kubuni mbinu za kujipatia kipato. Pia nitaviimarisha vikundi vya wanawake vilivyopo na kuwawezesha kupata mafunzo ya ujasiriamali na namna bora ya kujikwamua kiuchumi.

Maregesi ni nani?

Ana shahada ya kwanza ya uandishi wa habari aliyoipata kupitia Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT).

Alianza kazi ya uandishi wa habari mwanzoni mwa miaka ya 2000 akiwa mwandishi wa habari wa kawaida katika gazeti la Mwananchi. Baadaye aliamia gazeti la Mtanzania akiwa mwandishi wa kawaida, kisha akateuliwa kuwa mwandishi mkuu wa gazeti hilo.

Baadaye alipandishwa cheo na kuwa Mhariri wa Habari wa gazeti hilo, kisha akawa Mhariri Mkuu na baadaye akawa Mhariri wa Habari za mikoani katika gazeti hilo.

Baadaye aliamia katika gazeti la Tanzania Daima na kuwa Mhariri Mkuu.

Mwaka jana alijiunga na gazeti la Pambazuko kwa ngazi ya Mhariri wa Habari.

Mwaka 2010, aliripoti kampeni za uchaguzi mkuu akiwa na mgombea Urais wa CCM, Jakaya Kikwete na mwaka 2015, aliripoti kampeni za mgombea urais wa Chadema, Edward Lowassa.

Maregesi amekuwa mwandishi wa habari za Bunge kuanzia mwaka 2008 na mwaka 2014, aliripoti Bunge Maalumu la Katiba.

Kwa upande wa matukio makubwa aliyoripoti mwaka huu ni pamoja na mikutano mikuu maalumu ya CCM iliyofanyika Januari mwaka huu na Mei mwaka huu jijini Dodoma pia, aliripoti mkutano wa nishati uliowaleta jijini Dar es Salaam, marais wa Afrika.


Mitindo & Urembo**Suruali za jeje zinavyobamba**

SURUALI za jeje ambazo zinajulikana kama suruali za bwanga za vitambaa, ni aina ya vazi lenye mvuto mkubwa wa kiutamaduni na kisasa.

Vazi hili huvaliwa zaidi na wanawake katika maeeneo mengi ya nchi za Afrika.

Suruali hii huwa ni pana kuanzia kiunoni hadi miguuni na mara nyingi hutengenezwa kwa vitambaa maridadi kama kitenge, kanga au vitenge vya wax na siku hizi vipo vya staili ya jinsi pia.

Ili uonekane maridadi zaidi unapovaa vali hili hakikisha juu unatupia 'top' iliyobana kidogo.

**Unafahamu umuhimu wa kufanya scrub?**

KAMA ulikuwa hutumii scrub kwenye ngozi yako hasa ya uso, basi anza sasa kutumia.

Scrub ina faida nyingi kwa ngozi; kwanza inasaidia kuondoa seli za ngozi zilizokufa, hivyo huifanya ngozi yako ionekane iking'aa.

Pia hufungua pores (vinyweleo) vilivyoziba, kupunguza uwezekano wa chunusi na kumaliza matatizo mengine ya ngozi.

Mara nyingi ngozi ya uso inakuwa na uchafu ambao huwezi kuuona kwa macho na ule uchafu huwa unaenda kuziba vinyweleo na kufanya ngozi ishindwe kupumua vizuri, matokeo yake humfanya mtu aanze kutokwa na chunusi nyingi na mapele makubwa usoni.

Mambo ya kuzingatia;

*Osha uso wako na kuuacha na majimaji, kisha anza kupaka scrub na kusugua taratibu mfumo wa kuchora duara kwa dakika tatu au hadi tano.

*Ukimaliza nawa uso wako kwa maji mengi bila kutumia sabuni.

Tumia scrub mara mbili kwa wiki kwa siku zisizofuatana.





Na Anti
MSHAURI



Uhusiano

Tusiishi maisha ya kujikweza

HABARI za leo msomaji wa safu hii ya uhusiano ambayo hukupatia vionjo mbalimbali kuhusu maisha.

Leo nitazungumzia umuhimu wa kuchangamana katika masuala ya kijamii.

Itambulike kuwa kila mtu amejaaliwa uwezo na karama mbalimbali kimaisha.

Kuna ambao wamejaliwa uwezo wa kifedha, kwa maana kwamba hawapungukiwi na kuna waliojaliwa ujuzi na maarifa, lakini hawana uwezo mkubwa wa kifedha.

Kuna ambao pia hawana uwezo wa kifedha wala ujuzi wa aina yoyote; hao huishi tu ili mradi siku ziende na wapo ambao ni wa kawaida, lakini wamejaliwa maarifa ambayo huyatumia kupata riziki.

Pamoja na tofauti hizo za walionacho na wasionacho, lakini wote wanapaswa kuwa kitu kimoja bila kubaguana; tajiri amuone asiyenacho kuwa sawa naye.

Hakuna sababu ya mwenye nguvu ya kifedha kumuona asiyenacho kuwa hafai au hana haki ya kufanya chochote mbele yake.

Hiyo ni dhana mbaya kwani katika maisha ya sasa wapo watu wenye uwezo ambao hujiona bora kuliko wengine kwa kujivika vyeo vya juu na kusahau kuwa hayo ni mambo ya kupita.

Kuna ambao hudiriki

kubeza na kudharau wasionacho na kushindwa kujitoa kwao katika matukio ya kijamii yanayotokea kama vile misiba au sherehe.

Tunapaswa kusoma alama za nyakati kwa kuelewa kwamba shida haina mwenyewe, kwani pamoja na uwezo wa kifedha tunaajaliwa ipo siku matatizo ambayo utatuzi wake utahitaji nguvu ya umma utatokea na tunaowadharau leo watakuwa wa kwanza kutukimbilia.

Ni vyema tukafahamu kwamba pamoja na utajiri, vyeo na vitu vingine vya kifahari tulivyonayo, kuna maisha baada yote hayo.

Tunapaswa kuishi kwa kuheshimiana, kupendana, kuchukulina na kwa ushirika mzuri ili mwisho wa maisha yetu uwe mwenye hakuna ai juaye kesho yake.

Panapo majaaliwa ya Mola tukutane wiki ijayo.

Kwa maoni na ushauri:
hellen2ngoromera@gmail.com Au simu:
0715 88 67 49.



Burudani

'Chukuachukua' fomu za CCM kwa wasanii ni kiki au!

**Na Mwandishi WETU**

WAKATI pazia la uchukuaji fomu kuwania nafasi mbalimbali likifunguliwa ndani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuelekea Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, 2025, wasanii wa bongo fleva nao hawakuwa nyuma.

Wasanii wengi wameamua kujitosa kuomba ridhaa kwa chama hicho tawala ili waweze kuwakilisha wananchi bungeni au udiwani.

Mapema wiki iliyopita, msanii Harmonize alitangaza nia ya kugombea ubunge katika Jimbo la Tandahimba mkoani Mtwara.

Mbali na Harmonize, Barton Mwemba maarufu - Mwijaku pamoja na Baba Levo nao wamejitosa kunyeme-

lea Jimbo la Kigoma Mjini.

Kaka yake na Diamond Platnumz, 'Romy Jons' naye amejitosa kutaka kuwania Jimbo la Mbagala. Mwingine ni Nurdin Bilali, maarufu - 'Shetta' yeye ameomba nafasi ya udiwani katika Kata ya Mchikichini, Dar es Salaam.

Wafuatiliaji wa mambo hasa ya uchaguzi, wanahoji kwamba je, wasanii hao wako 'serious' au ni kiki tu?

Wanahoji zaidi kwamba je, wamejipima kama wanatosha au ndio wanafuata kiki tu za mitandaoni?

Pamoja na kwamba Katiba inawaruhusu kwa kila mtu kuwa na haki ya kugombea, lakini wanafahamu kweli kazi na wajibu wa mbunge na udiwani au ndio funika kombe mwanaharamu apite.

Chid Benz anakula 'mchele' siyo unga tena

Na Mwandishi WETU

MSANII wa Bongo Fleva, Rashid Makwiro 'Chid Benz' ameachana na matumizi ya dawa za kulevya na kurejea katika afya yake ya awali.

Chid Benz alionekana hivi karibuni kwenye kilele cha siku ya dawa za kulevya ambapo kitaifa ilifanyika mkoani Dodoma, huku akipata fursa ya kutumbuiza mbele ya Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa.

Msanii huyo amekuwa akidaiwa kuwa na tabia ya kuacha na kurejea kwenye matumizi ya dawa hizo mara kwa mara tangu 2014 na kuonekana kama sikio la kufa.

Binafsi amekuwa akikiri kufanya hivyo, ingawa safari hii huenda "amemaanisha." Swali ambalo watu wengi wanajiuliza je safari hii Chid ameamua kuacha kabisa dawa hizo au atarejea tena?

Pambazuko tunamuomba kwa Mwenyezi Mungu ampe afya njema na arejee tena kwenye



kazi zake za muziki kama zamani kwani mashabiki wana kiu ya kupata kazi mpya.

Michezo

Vigogo wapongeza Yanga

Na Hellen NGOROMERA, Dodoma

UBINGWA wa historia wa Timu ya Yanga kui-buka kinara wa soka Tanzania, kuliibua sham-rashamra bungeni, huku Waziri wa Fedha, Dkt. Mwigulu Nchemba, akitumia ushindi huo kunanga mashabiki wa Klabu ya Simba.

Jumatano iliyopita, Yanga ilitawazwa kuwa bingwa wa soka Tanzania Bara baada ya kuifunga Simba 2-0 katika mechi ya mwisho ya Ligi ya NBC, iliyopigwa katika Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam.

Hii inakuwa mara ya nne mfululizo kwa Yanga kutwaa ubingwa huo.

Akizungumza bungeni, Dkt. Nchemba alisema ushindi huo wa mara nne mfululizo kwa Yanga, umeitupa kando Simba katika ramani za ubingwa wa ligi kuu kwani haijawahi kushuhudiwa na mtoto aliyehitimu kidato cha nne mwaka huu tangu aanze masomo ya sekondari.

Waziri Nchemba alisema hayo mwishoni mwa wiki wakati akihitimisha hoja kuhusu azi-

mio la Bunge kuridhia mkataba wa uanzishwaji wa Shirika la Fedha la Afrika la mwaka 2007.

“Mheshimiwa Spika, Siku ya Jumatano, tarehe 25 kulikuwa na shughuli kubwa, lakini shughuli bado inaendelea ila lazima niseme ni Yanga tena...” “Kwa takwimu za jana, ni dhahiri mtoto aliyeanza form one (kidato cha kwanza) hadi form four (kidato cha nne), hajaona ubingwa wa Simba,” alisema Nchemba huku akishangiliwa na wabunge.

Hali kadhalika, Spika wa Bunge, Dkt. Tulia Akson, naye alijiunga na Nchemba kuipongeza Yanga kwa kutwaa ubingwa huo na kuitaka kuvitumia pia viwango walivyovionyesha wachezaji wake kupata ubingwa huo katika michuano ya kimataifa.

Kwa upande wake, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, wakati akihitimisha hoja yake ya kua-hirisha Bunge, alitumia wasaaa huo kupongeza Yanga kwa kutwaa ubingwa huo na klabu ya Simba kwa kupambana mpaka mechi ya mwisho na kuongeza ladha ya ligi hiyo.

Majaliwa pia aliipongeza klabu ya Simba kwa hatua kubwa ya kutinga fainali katika Kombe la Shirikisho Afrika kwa msimu wa 2024/2025.

Soka kumpa ubunge Hersi

Inatoka Uk. 40

Matutu pamoja na wachambuzi wengine wa soka wanaeleza kuwa endapo Mhandisi Hersi atachaguliwa kuwa mbunge, dhamana hiyo hai-tatokana na mashabiki wa Yanga pekee, bali wa-nanchi wa Kigamboni, ambao wanaamini katika uongozi wake.

Kwa Tanzania, viongozi wengi wanabebwa na wafuasi na mashabiki wengi wa mifumo ya Imani, ambao wameegamia kwenye dini, michezo – hasa soka na vyama vya siasa.

Mifumo hiyo mitatu ndiyo inayoongoza kufuatiliwa na kupendwa na idadi kubwa ya Watanzania, bila kujali rika.

Wanaofuatilia mifumo mingine ya maisha; ikiwamo muziki wa kisasa; Bongo Flewa, ule wa “kufokafoka” na hata singeli, ni vijana zaidi, wengi wakiwa ni wenye umri kuanzia miaka 12 hadi 32. Hata hivyo, katika kuweka mizania ya wingi wa idadi ya wapenzi, dini ndiyo inaongoza kua-

miniwa na watu wengi, huku soka ikifuata na baadaye siasa.

Ukicha dini, ambayo iko kwenye misingi ya imani zaidi, soka inapewa msukumo wa ushawishi na mapenzi ya mtu mmoja mmoja na hata makundi ya watu ambao hubeba ushabiki mkubwa, ambao pengine uhama kutoka kwenye timu na kugusa wachezaji na hata viongozi wa timu wanazoshabikia – hasa zinapofanya vyema uwanjani na kuibuka washindi.

Ni kwa msingi huo, soka la Tanzania linaweza kutajwa kuwa ni “taifa ndani ya taifa.”

Taifa hilo la soka katika Tanzania liko kwenye timu mbili kubwa; Simba na Yanga, ambazo licha ya kuwa na historia inayokwenda sambamba na uhuru na hata maendeleo ya nchi, na kujenga furaha zinazopitiliza. Hivi sasa – kwa maana ya wanachama na aNi kutokana na ambao soka ni Ikulu inatambua kuwa timu kubwa za Simba na Yanga zinabeba nguvu zenye ushawishi mkubwa – siyo tu kwenye soka, bali hata kijamii na kisiasa.



Soka kumpa ubunge Hersi



Na Mwandishi WETU

UPO uwezekano mkubwa kwa Rais wa Klabu ya Yanga, Mhandisi Hersi Ally Said, kuwemo katika orodha ya viongozi wa klabu kubwa za soka Tanzania; Simba na Yanga ambao waliwania nafasi za kisiasa na kuibuka washindi.

Mhandisi Hersi tayari mwishoni mwa wiki iliyopita, alichukua fomu ya kuomba kuteuliwa na chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kuomba ridhaa ya wanachama kuwania kiti cha Ubunge Jimbo la Kigamboni, Dar es Salaam.

Endapo Mhandisi Hersi, atafanikiwa kupeperusha bendera ya CCM katika kuwania

nafasi hiyo, atachuana na wagombea wa vyama vingine katika uchaguzi mkuu unaotarajiwa kufanyika baadaye mwaka huu.

Ikiwa atashida dhamana hiyo ya uwakilishi wa kisiasa, Mhandisi Hersi atakuwa amepeny kupitia jukwaa la soka, ambalo limewabeba wengi waliomo kwenye nafasi za ubunge au waliowahi kuwamo bungeni.

Miongoni mwa “waliobebwa” na soka hadi kuwa viongozi wa kisiasa ni pamoja na Mohammed Dewji – mmiliki wa sasa wa Simba, aliyekuwa Mbunge wa Singida Mjini (CCM), Abbas Gulamani – aliyewahi kuwa mfadhili mkuu wa Klabu ya Yanga - Mbunge wa Kilombero (CCM); Tarimba Gulam Abbas- Mbunge wa sasa wa Kinondoni (CCM) – aliwahi kuwa kiungozi wa Yanga; Murtaza Ally Mangungu – Mwenyekiti wa Klabu ya Simba - Mbunge wa Kilwa Kaskazini na wengine wengi.

Wengine ni Ismail Aden Rage, aliyekuwa Mbunge wa Tabora Mjini (CCM), baada ya kubebwa na umaarufu wa Klabu ya Simba akiwa mwenyekiti wa timu hiyo, pia kwenye orodha hiyo yumo Juma Suleman Nkamia, ambaye alikuwa mkereketwa mkubwa wa Simba.

“Naomba nikueleze kuwa mimi siyo mpenzi wa Yanga, nashabikia Simba, lakini napenda namna uongozi wa Yanga unavyofanya kazi, hasa injinia Hersi anavyoiweka timu yake kiungozi, sasa ikiwa anaiweza Yanga, hawezi kushindwa jimbo, akipitishwa na CCM, kura yangu anayo,” amesema Ali Matutu, mkazi wa Kigamboni.

Inaendelea Uk. 39